epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Jumatatu Septemba 30, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581815
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA 22

NYOTA WANNE WANAOWEZA KUVAA VIATU VYA RODRI CITY



Watuhumiwa wanne wa kesi ya kushiriki katika ubakaji wa genge ambao hukumu yao inatarajiwa kutolewa leo na Mahakama ya Hakimu Mkazi Dodoma. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Hatima washtakiwa kesi ya 'Binti wa Yombo' leo

UKURASA 15

**WAKITIWA HATIANI...**

*Kila mtu ambaye ana hatia ya kubaka kwa kikundi, atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha maisha"*
*Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sira 16, Kifungu cha 131A (2)*

*"Mtu yeyote ambaye atashambulia kwa kusudi la kujamiiana na mtu yeyote kinyume cha maumbile, atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka 14"*
*Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura 16, Kifungu cha 290 (1) (c) (iii)*

## Madhila wapatayo wanafunzi wa kike wanaoshi 'ghetto'

UKURASA 4

UKURASA WA 2

**IPP** Media yang'ara tena tuzo za EJAT

UKURASA WA 3

**Kicheko** Mikopo ya Elimu ya Juu, orodha ya kwanza wanufaika yatoka



UKURASA WA 15

**Punda**, mbwa waondolewa katika orodha ya wanyama wanaoliwa



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule.

TOLEO MAALUM

## Fursa tele uwekezaji kila kona Dodoma

UK. I & II

**MICHEZO** **KIBU AITAMANI MECHI YANGA MAPEMA** UK.24

**KATUNI** UK.6

# ACT yataka serikali kutatua tatizo la maji Kanda ya Ziwa

**Na Halfani Chusi**

KATIBU Mkuu wa Chama cha ACT Wazalendo, Ado Shaibu ameitaka serikali ihakikishe upatikanaji maji kwa wananchi wa Kanda ya Ziwa unakuwa wa uhakika, akisisitiza hakuna sababu ya ukanda huo kukosa huduma hiyo huku wakiwa wanazungukwa na Ziwa Victoria.

Ziwa Victoria ni la pili kwa ukubwa lenye maji baridi likiwa katika nchi za Tanzania, Kenya, Uganda na kwamba sehemu kubwa ya maji ipo nchini kwa asilimia 49.

Kiongozi huyo alisema licha ya kuwapo rasilimali hiyo, wananchi wa kanda ya ziwa wanalalamika shida ya maji, wakichangia maji na mifugo.

"Ni aibu kwa serikali ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) watu wa Kanda ya Ziwa wanaoishi kando ya ziwa Victoria hawana uhakika wa maji, ni aibu sana hii ni ishara kwamba wananchi wa Buchosa mmepuuzwa," alisema.

Ado aliyasema hayo alipohutubia wananchi wa Buchosa, mkoani Mwanza jana akiwa kwenye mwendelezo wa ziara yake Kanda ya Ziwa ikijumuisha mikoa ya Simiyu, Mara, Mwanza, Geita na Kagera.

Alisisitiza msimamo wake wa kuendelea kupigia kelele suala la upatikanaji mbolea kwa wakati na kiwango stahiki kwa wakulima.

Katibu Mkuu pia alisema mbolea ya ruzuku ya serikali inauzwa kwa Sh. 70,000 wakati mbolea isiyo ya ruzuku inauzwa kati ya Sh. 140,000 mpaka 150,000.

Vilevile, alilamikia ukosefu wa vivuko vya uhakika kwenda na kurudi kwenye visiwa mbalimbali vilivyo katika Ziwa Victoria. Alisema wananchi wa eneo hilo wanalalamika kukosa vivuko vya uhakika na kulazimika kuvuka kwa kutumia ngarawa kutoka Buchosa kwenda visiwa vya Gambare, Kasarazi, Nyamango, Soswa, Soswa, Kembaya na Kamagati, wakilipa nauli kubwa.

"Tunataka wananchi wa Buchosa wapate vivuko vya uhakika, Rais Samia Suluhu Hassan anasikia na viongozi wengine wanasikia," alisema Ado.

Kiongozi huyo anaendelea na ziara yake katika mikoa ya Kanda ya Ziwa ya kuyafikia majimbo 214 kuyaandaa kwa ajili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.



Mhariri Mtendaji wa gazeti Nipashe, Beatrice Bandawe (wa tatu kulia), akifurahia jambo na waandishi wa habari wa IPP Media walioshinda Tuzo za EJAT 2023, jijini Dar es Salaam juzi. Kutoka kushoto Halfani Chusi (Nipashe), Christina Mwakangale (Nipashe), Benjamin Mzinga (ITV), Saimon Rodgers (ITV) na Sanula Athanas (Nipashe). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waandishi wa IPP wang'ara tena tuzo umahiri wa uandishi habari

**Na Mwandishi Wetu**

WAANDISHI wa habari saba kutoka kampuni za IPP Media wametambuliwa na kutunukiwa Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) wakati wa hafla ya utuzaji tuzo hizo iliyoandaliwa na Baraza la Habari Tanzania (MCT) jijini Dar es Salaam.

Katika hafla hiyo iliyofanyika juzi, Msanifu Mkuu wa gazeti Nipashe, Sanula Athanas alibuka mshindi katika kipengele cha Habari za Elimu ambacho alishinda nafasi ya kwanza na ya pili upande wa magazeti.

Ripoti maalum kuhusu shule za nyasi wilayani Tunduru, mkoani Ruvuma iliyoripotiwa na gazeti hili Novemba mwaka jana ndiyo iliyotambuliwa na majaji wa tuzo hizo kuwa habari bora zaidi ya elimu kwa mwaka 2023 upande wa magazeti, ikifuatiwa na ripoti kuhusu 'Wilaya ya Bunda na maisha hasi kwa watoto' iliyochapishwa na Nipashe mwezi huo huo mwaka jana.

Sanula, ambaye alikuwa Mshindi wa Jumla wa EJAT 2022, pia alitangazwa mshindi katika kipengele cha Kundi la Wazi, ambacho pia alishika nafasi ya kwanza na ya pili upande wa magazeti.

Ripoti ya uchunguzi kuhusu mkasa wa mjamzito kubakwa na hatimaye kufungwa katika kiroba wilayani Mkuranga, mkoani Pwani mnamo Juni 5 mwaka jana, ndiyo iliyotambuliwa na majaji wa EJAT 2023 kuwa habari bora zaidi kwa mwaka huo upande wa magazeti katika kundi hilo, ikifuatwa na ripoti nyingine ya Sanula kuhusu 'Maisha mapya ya wananchi wa Ukerewe, makazi na mashamba yakimezwa na ziwa'.

Sanula pia alipenya katika orodha ya waandishi wa habari watatu ya kumsaka Mshindi wa Jumla wa EJAT 2023, ikiwa ni mara ya nne mfululizo, akiingia katika kinyang'anyiro hicho kuanzia mwaka 2020.

Mwandishi wa habari wa Nipashe mkoani Dar es Salaam, Halfani Chusi, aliibuka mshindi katika kipengele cha Habari za Haki za Binadamu na Utawala Bora kutokana na ripoti yake ya uchunguzi kuhusu mkasa wa 'Askari-pori kudhuru wananchi Mbarali' kutokana na mgogoro wa kimpaka kati ya wanakijiji na Hifadhi ya Taifa Ruaha.

Christina Mwakangale, mwandishi mwingine wa Nipashe mkoani Dar es Salaam, alishika nafasi ya pili katika kipengele cha Mwandishi Bora wa Habari za Ulinzi wa Vyanzo vya Maji na Mazingira.

Ripoti kuhusu hali ya dampo la Pugu, jijini Dar es Salaam, ndiyo imembeba Christina kushinda tuzo hiyo upande wa magazeti.

Saimon Rogers na Benjamin Mzinga, wote wa ITV, waliibuka washindi katika kipengele cha Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa upande wa luninga, wakishirikiana kuandaa ripoti maalum kuhusu 'Watoto kula makombo ya mifupa ya nyama mnadani jijini Dodoma'.

Mshindi wa jumla wa tuzo hizo ni Mukrim Mohamed Khamis wa KTV TZ, akiweka rekodi kwa kuwa Mshindi wa Jumla wa kwanza kutoka Zanzibar katika historia ya tuzo hizo zilizotolewa kwa miaka 15 mfululizo.

Akizungumza wakati wa tuzo hizo, mgeni rasmi Naibu Waziri, Mussa Zungu, aliyemwakilisha Spika wa Bunge na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), Dk. Tulia Ackson, alisema waandishi wa habari waendelee kujikita katika uandishi wa habari za weledi na usahihi, ili kuondoa migongano katika jamii na uvunjifu wa amani.

"Hakuna utafiti, hakuna haki ya kuongea. Uandishi ni zaidi ya upanga halisi, kalamu isipotumika vizuri inaweza kuvunja amani ya nchi. Waandishi mjikite katika ukweli hasa katika dunia ya sasa iliyokua kiteknolojia," alisema Zungu.

Pia aliwataka wadau wa habari nchini kuwasilisha serikalini sheria au vifungu vya sheria visivyokidhi matamanio ya waandishi wa habari ili vipelekwe bungeni kufanyiwa kazi.

"Bunge liko tayari kuweka mazingira wezeshi ili wanahabari kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Serikali ni sikivu na Bunge litatenda haki, ili kukidhi matakwa ya wananchi, wanahabari ni sehemu yao.

"Bunge liko tayari kuboresha sheria ili kuwa na mazingira rafiki na wezeshi ili waandishi wa habari kufanya kazi zao kwa weledi," alisema.

Zungu pia aliwapongeza waandishi wa habari walioikidhi vigezo vya kuteuliwa kuwania tuzo hizo baada ya kupita katika mchujo wa jopo la majaji lililoongozwa na Halima Sharif.

Mwenyekiti wa Jopo la Majaji wa EJAT 2023, Halima, alisema kuna changamoto kadhaa zilijitokeza wakati wa kuzifanyia uchambuzi habari zilizowasilishwa zinazofikia 1,135, ikiwa ni pamoja na kujikita zaidi na vyanzo vya mikutano ya waandishi wa habari.

"Habari nyingi zilikuwa zimetokana na 'press conference' alisema... miongoni mwa vigezo tulivyozingatia ni habari zilizo na vyanzo sahihi na mahususi. Ni vyema habari izingatie vyanzo vyenye usahihi," alisema Halima.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya tuzo hizo, Ernest Sungura, alisema kuna ongezeko la kazi zilizowasilishwa mwaka 2023 zilizofikia 1,135 kutoka kazi 893 za EJAT 2022.

Sungura ambaye pia ni Katibu Mtendaji wa MCT, alisema kazi za EJAT mwaka 2020 zilikuwa 396 na EJAT 2021 zilikuwa 608.

Alisema kuwa katika kazi za EJAT 2023, waandishi wa habari wa Mkoa wa Dar es Salaam wameongoza kwa kuwasilisha kazi 290, wakifuatiwa na Arusha (81), Mwanza (74) huku Iringa ikishika nafasi ya nne kwa kuwa na kazi 72.

Mkoa wa Mtwara ulishika nafasi ya tano kwa kuwa na kazi 49 huku kwa upande wa Zanzibar, kazi zilizopokewa ni kutoka Kaskazini Pemba (36) Pemba Kusini (43) na Mjini Magharibi (29).

Kati ya waandishi 72 walioshiriki kinyang'anyiro juzi, walituzwa tuzo za umahairi katika uandishi wa habari, wakijumuisha wanaume 45, sawa na asilimia 62.5 na wanawake ni 27 sawa na asilimia 37.5.

Sungura alisema kuwa kati ya wateule hao, 14 walitoka katika runinga, 13 vyombo vya mtandaoni, redio 20 na wateule 25 walitoka kwenye magazeti.

## HABARI KITAIFA

# Kicheko mikopo ya elimu ya juu

### -HESLB yaanza kutoa orodha ya wanufaika 2024/2025

Na Mwandishi Wetu

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imeanza kutangaza orodha ya wanafunzi wenye sifa waliopangiwa mikopo kwa ajili ya mwaka wa masomo 2024/25, 'kicheko' kwa wanufaika kikiwa ni kupanda kwa kiwango cha chini cha mkopo kwa mnufaika mmoja mmoja hadi Sh. milioni tatu kutoka Sh. milioni 2.7 mwaka uliopita wa masomo.

Awamu hii ya kwanza ya wanufaika hao iliyotangazwa juzi, inajumuisha wanafunzi wa mwaka wa kwanza waliopangiwa mikopo ya shahada ya awali, shule ya sheria kwa vitendo na shahada ya uzamili.

Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dk. Bill Kiwia, akizungumza na waandishi habari jijini Dar es Salaam juzi, alisema wanafunzi wote walioomba mikopo kwa mwaka 2024/25 wanaweza kupata taarifa za kina kuhusu mikopo yao kupitia akaunti walizotumia kuombea mikopo, maarufu SIPA, yaani 'Student's Individual Permanent Account'.

"Leo (juzi) tumeanza kutoa taarifa za mikopo kwa makundi yote, waliopangiwa mikopo, wapo ambao bado tunaendelea kufanyia kazi maombi yao kila mwombaji anapata taarifa yake kwenye akaunti ileile aliyotumia kuombea mkopo, huhitaji kufika ofisi za HESLB", alisema Dk. Kiwia na kuongeza kuwa upangaji mikopo kwa wanafunzi wa stashahada na shahada ya uzamivu unaendelea.




Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dk. Bill Kiwia (kulia) na Rais wa TAHLISO, Zainab Kitima.

Dk. Kiwia alisema kuwa HESLB imeanza kuandaa malipo ya wanafunzi wapya na wanaoendelea na masomo ambao ni wanufaika wa mikopo na kusema kuwa lengo ni kuhakikisha fedha zinafika vyuoni kwa wakati.

"Mwaka huu, serikali imetenga Sh. bilioni 787 kwa ajili ya jumla ya wanafunzi 245,799 wakiwamo zaidi ya wanafunzi 88,000 wa mwaka wa kwanza waliotengewa Sh. bilioni 284.8, alisema Dk. Kiwia na kuongeza kuwa bajeti ya mwaka 2024/25 imeongezeka kwa Sh. bilioni 38 sawa na asilimia 5.1 kulinganishwa na bajeti ya 2023/24 iliyokuwa Sh. bilioni 749.4.

Mkurugenzi huyo alibainisha kuwa mwaka huu, kiwango cha chini cha mkopo kwa mnufaika mmoja mmoja kimepanda hadi Sh. milioni tatu kutoka Sh. milioni 2.7 mwaka jana (2023/24).

Kuhusu wajibu wa vyuo, Dk. Kiwia alikumbusha vyuo ambavyo havijawasilisha matokeo ya mitihani ya wanafunzi-wanufaika wanaoendelea na masomo, kuwasilisha ili kuwezesha HESLB kuandaa malipo kwa wakati.

"Kuna vyuo vichache ambavyo bado havijawasilisha matokeo, tumewakumbusha na tunasisitiza waharakishe kuwasilisha matokeo ili tukamilishe malipo ya wanafunzi waliofaulu kuendelea na masomo," alisema Dk. Kiwia.

Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB alisema kuwa awamu ya pili ya orodha ya wanafunzi waliopangiwa mikopo kwa mwaka 2024/25 itatangazwa wiki ijayo.

Vilevile, Dk. Kiwia alieleza kuwa elimu iliyotolewa kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari nchini kuhusu namna ya kuomba mikopo, imesaidia kupunguza makosa ya waombaji, hivyo kuharakisha mchakato wa kuwapangia mkopo.

Rais wa Jumuiya ya Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu na vya Kati (TAHLISO), Zainab Kitima, alishukuru serikali kwa jitihada zake za kuongeza kiwango cha chini cha mkopo kwa mnufaika mmoja mmoja, akifafanua kuwa ongezeko hilo limepunguza mzigo kwa wazazi na wanafunzi, hasa kutoka familia zenye hali duni.

"Tunaishukuru sana serikali. Leo tumemsikia Mkurugenzi Dk. Kiwia akisema mikopo itafikishwa vyuoni kwa wakati, jambo ambalo ni faraja kwa wanafunzi wa mikopo kote nchini.

Hata hivyo, tunaendelea kutoa wito kwa HESLB kuzingatia changamoto zingine ambazo bado tunazo," alisema Zainab.

Mwongozo utoaji mikopo na ruzuku ulizinduliwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda Mei 27 mwaka huu. Dirisha la uombaji mikopo lilifunguliwa Juni Mosi na kufungwa Septemba 14 mwaka huu.


## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

AngloGoldAshanti
Geita Gold Mining Limited

PO Box 532, Geita, Tanzania
Tel: + 255 282 160 100
Fax: +255 282 160 104
Dar es Salaam Office:
1st Floor, Mkumi House, Plot No.368, Msasani Road,
Oysterbay, Kinondoni District
PO Box 75803, Dar es Salaam, Tanzania
Tel: + 255 222 926594/255222926597/255222926599
Fax: + 255 222 926598
Website: www.anglogoldashanti.com

## GGML Yatoa 200,000,000/= Kudhamini Maonesho ya 7 ya Teknolojia ya Madini Geita.

Geita Gold Mining Limited (GGML) kampuni tanzu ya AngloGold Ashanti imeonyesha tena dhamira yake ya kuendeleza ubunifu na maendeleo kwa kudhamini Maonesho ya 7 ya Teknolojia ya Madini kwa kutoa msaada wa **Shilingi Milioni Mia Mbili (200,000,000/=)**. Maonesho haya ya kila mwaka yanayotarajiwa kufanyika kuanzia tarehe 02 hadi 13 Oktoba 2024 ni jukwaa la kibiashara linalokutanisha wadau kutoka sekta mbalimbali, likitoa fursa kwa GGML kuonyesha uvumbuzi wake wa kiteknolojia, uzingatiaji wa maudhui ya ndani na uwekezaji katika jamii kupitia Uwajibikaji kwa Jamii wa Kampuni (CSR).

Maonesho haya ni jitihada za pamoja kati ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Geita na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) yakifanyika katika viwanja vya EPZA huko Geita, kituo ambacho pia kilijengwa na GGML kupitia mipango yake ya kina ya Uwajibikaji kwa Jamii wa Kampuni (CSR).

Gilbert Mworia, Meneja Mwandamizi wa Uendelevu wa GGML, alitoa maoni kuhusu ushiriki wa GGML katika maonesho hayo akisema, "GGML imekuwa ikishiriki na kudhamini maonesho haya kwa miaka saba mfululizo katika ushirikiano huu na inafurahia kuonyesha ujuzi na uvumbuzi wa kiteknolojia katika sekta ya madini. Mchango wetu ni zaidi ya msaada wa kifedha, tunajitahidi pia kuimarisha mahusiano na mamlaka ya serikali za mtaa, biashara za ndani, wachimbaji wadogo, na jamii kwa ujumla," alisema Mworia..

Kwa mujibu wa lengo lake la muda mrefu la maendeleo endelevu, GGML inaunga mkono kwa dhati Dira ya Serikali ya Tanzania ya 2025, inayolenga sekta ya madini kuchangia angalau asilimia 10 ya Pato la Taifa.

Ufunguzi rasmi wa Maonesho ya 7 ya Teknolojia ya Madini mkoani Geita utahudhuriwa na Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko (Mb), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, tarehe 05 Oktoba 2024, na kufungwa tarehe 13 Oktoba 2024, na Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Tangu kuanzishwa kwake mwaka 2000, GGML imeendelea kusimama imara katika kusaidia ustawi na maendeleo ya jamii inayoizunguka. Kupitia miradi ya afya, elimu hadi miundombinu na miradi ya ujasiriamali, kila mwaka, GGML huwekeza fedha na rasilimali katika juhudi zake za kudumu za Uwajibikaji wa Jamii wa Kampuni (CSR) ili kuendelea kuimarisha jamii ya Geita na Tanzania kwa ujumla.




Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Isagenhe,wilayani Nzega mkoani Tabora wakionesha bango kufikisha ujumbe kuhusu vikwazo wanavyopitia kufikia ndoto zao. **PICHA:ELIZABETH ZAYA**

# Machungu wanayopitia wanafunzi wanaoishi 'ghetto'

**Na Elizabeth Zaya,** TABORA

NDOTO za wanafunzi wa Shule ya Sekondari Isagenhe, wilayani Nzega, mkoani Tabora kufika katika hatua nzuri kielimu, zinasongwa na vikwazo lukuki.

Kutokana na kutembea umbali mrefu kutoka nyumbani kwenda shuleni, wanafunzi hao waliamua kupanga vyumba, maarufu ghetto, katika kijiji cha Isagenhe, kilichoko karibu na shule yao.

Kwa nyakati tofauti, wanafunzi hao wanaelezea hali halisi ya maisha ya ghetto kwa mwandishi wa habari wa Nipashe aliyeko katika ziara ya wadau wa Mtandao wa Kutokomeza Ndoa za Utotoni Tanzania (TECMN) waliofika katika kijiji hicho kutoa elimu ya namna ya kupambana na ukatili na ndoa za utotoni ili kumpa fursa mtoto wa kike kutimiza ndoto zake.

Wanafunzi hao wameelezea namna ambavyo maisha ya gheto yamegeuka kuwa mzigo kwao, hata kutamani kurudi kuishi nyumbani kwa wazazi wao, lakini wanawaza madhila ya kutembea umbali mrefu waliyopitia kabla ya kuamua kuishi maisha hayo ya ghetto.

Lengo la kuingia katika maisha hayo ya ghetto lilikuwa jema - kupunguza umbali ambao wamekuwa wakitembea kwenda shuleni na kurejea nyumbani, huku wakikumbana na vikwazo katika safari zao za kila siku, ikiwamo kunusurika kuliwa na wanyama wakali.

Si tu wanyama wakali, kutembea umbali mrefu kwenda shule na kurejea nyumbani, kuliwaweka katika hatari ya kubakwa na watu wasio na nia njema.

Wakati mwingine, walifika shuleni kwa kuchelewa na kukosa baadhi ya vipindi vya masomo yao.

Kama hiyo haitoshi, madarasa yenye mitihani wanaotakiwa kurudi shuleni kwa ajili ya masomo ya ziada jioni kutokana na umbali wanakoishi walishindwa kuhudhuria.

Sasa wameamua kusogea karibu na shuleni ili kupunguza hatari zilizopo katika kutembea umbali mrefu, lakini bado ni kama shida zimeongezeka, wanakumbana na maisha magumu ya kuishiwa chakula na kushindwa kumudu pango la nyumba.

Wanajitwisha mzigo wa kujilea kwa kufanya vibarua mbalimbali vya muda mfupi, ili wapate fedha kwa ajili ya mahitaji ya kulipa pango la nyumba wanakoishi wakati wanaendelea na masomo, kununua chakula na mahitaji mengine kama madaftari.

Vibarua wanavyofanya ni pamoja na kazi za ndani kwenye nyumba za watu, kulea watoto na hata kufanya shughuli za shambani na siku wanazofanya hivyo mara nyingi ni zile za mapumziko, Jumamosi na Jumapili.

Na pale inapobidi, baadhi hutoroka vipindi shuleni, hata katikati ya wiki, muda wanaotakiwa kuwa darasani na kwenda kufanya vibarua hivyo, ili wapate fedha ya chakula na pango au kulipia mahitaji mengine hasa kunapokuwa na uhitaji wa haraka.

Ujira wa kazi hizo za vibarua kwa siku huanzia Sh. 2,000 hadi 4,000 kulingana na aina ya kibarua chenyewe.

Baadhi ya wanakijiji wanaelezea kwamba pamoja na wanafunzi hao kufanya vibarua kwa ajili ya kujitafutia fedha ya kujikimu, kumekuwa na 'mitego' inayowaweka kwenye hatari kubwa wanafunzi wa kike ya kushawishika kuingia katika uhusiano wa kimapenzi na hata kupata ujauzito.

Neema Julius ni miongoni mwa kinamama wanaoishi katika kijiji hicho anayesema wapo baadhi ya wanafunzi wa kike waliowahi kuishi maisha ya gheto, lakini walipewa ujauzito na wanaume walikokuwa wanafanya vibarua.

"Waliwahi kuja hapa wanafunzi wakapanga kama hivyo vyumba vyao kwa sababu walikotoka ni mbali, lakini wengi wao huwa wazazi wao hawawatumii fedha ya kujikimu, kwa hiyo wanalazimika kufanya vibarua lakini isivyo bahati wanakutana na kinababa wengine si watu wazuri, wanawarubuni kimapenzi kwa kuwapa fedha kidogo lakini mwisho wa siku wanaishia kupata mimba," anasema Neema.

**WANAFUNZI**

Mmoja wa wanafunzi wa kike anayesoma kidato cha pili katika Shule ya Sekondari Isagenhe, anayeishi maisha hayo ya ghetto (jina linahifadhiwa), anasema pamoja na kukosa fedha ya pango, chakula na mahitaji mengine ya shule, baadhi ya vijana pamoja na kinababa kijijini huko huwavizia kwenye ghetto mara kwa mara wakiwataka kimapenzi.

"Dada sijui nikwambieje... hapa si kukosa fedha tu, lakini kila siku tunaishi maisha ya kuviziwa, wanaweza kukufuata unapoishi au wakakutegea wakati unakwenda kwenye masomo ya 'prepo' au wakati unarudi.

"Unakuta vijana wamekaa kwenye vikundi, ukipita wanakufuatilia nyuma, wanakutongoza na ukikataa sasa, hayo matusi wanayokutukana kuna wakati unatamani uache na shule yenyewe urudi kijijini kwenu," anasema.

Anasema kuwa kwa sasa wanafunzi wote wanaopanga wameanzisha utaratibu wa kutembea kwa makundi wanapokwenda shuleni na kurejea, hasa wanapokwenda kwenye vipindi vya masomo vya usiku 'prepo'.

"Kuna mwenzetu mmoja naye alikuwa anapanga kama sisi, mwaka jana alikuwa kidato cha pili, lakini yeye amepata ujauzito na ni kwa sababu ya maisha magumu ya kuhangaika kutafuta fedha ya kujikimu na vishawishi vya kimapenzi, alishindwa kuvishinda.

"Vyumba tunavyopanga sisi kodi ni Sh. 5,000 au 10,000 kwa mwezi, kwa hiyo mzazi anaweza kukulipia ya mwezi mmoja au miwili lakini miezi inayofuata halipi na wala hajali kufuatilia unaishije, kwa hiyo kuna wakati unachanganyikiwa, unajikuta kila kitu kimeisha, huna fedha, pango, chakula, madaftari yameisha, darasani hapakaliki inabidi utoroke ukatafute kibarua na wengine ndio kama hivyo wanaona watafute wanaume wawasaidie ndio hao sasa wanapata mimba," anasimulia.

**MKUU WA SHULE**

Mkuu wa Shule ya Sekondari Isagenhe, Jumamne Shaban, alisema moja ya changamoto kubwa wanazokutana nazo ni wanafunzi kutembea umbali mrefu; wapo wanaosafiri umbali wa kilomita 20 kwenda shuleni, hivyo kwa siku moja anatembela kilomita 40.

"Chukulia mtoto huyu kama hana baiskeli, atafika saa ngapi shuleni akiwa anatembea kwa miguu? Maana si wote wenye hizo baiskeli na ndio maana huwa tunawashauri wazazi wawapangie vyumba maeneo ya karibu na shuleni wakati tukisubiri na kuweka tumaini kwamba mabweni yatajengwa," anasema Shaban.

Mwalimu huyo anabainisha kuwa mwaka 2017 hali ilikuwa mbaya zaidi na kwamba kutokana na wanafunzi wengi kutembea umbali mrefu, wapo waliokata tamaa na kukatisha masomo na ni wanafunzi wa kike wanne pekee ndio walifanikiwa kuhitimu kidato cha nne.

Anasema kuwa sasa wanapata hamasa kidogo kwa sababu wamesaidiwa baadhi ya mahitaji na Shirika la Msichana Initiative, zikiwamo baiskeli, sare za shule na daftari japo si wote ambao wamepata.

**SERIKALI**

Kaimu Ofisa Mtendaji wa Kata ya Isagenhe, Bajati Kalamu, alisema mwaka jana waliwakamata na kuwachukulia hatua baadhi ya watu waliobainika kuwashawishi wanafunzi wanaopanga mtaani kuanzisha nao uhusiano wa kimapenzi.

Mwaka jana tulibaini kwamba wapo baadhi ya watu wanaanzisha uhusiano wa kimapenzi na wanafunzi waliopanga mtaani na tuliwakamata, tukachukua hatua.

"Kwa sasa tumeomba walimu wawe na rekodi ya watoto waliopanga ili kuwafuatilia zaidi na kufahamu maendeleo yao," anasema Kalamu.

Anasema mpango wa serikali ni kujenga mabweni ili wanafunzi wote waishi shuleni badala ya kukaa mtaani na kwamba uhitaji uliopo ni mabweni manne.

"Na tumeomba wenyeviti wote wa vijiji wa kata hii, waitishe vikao na wananchi ili wenye uwezo wa kuchangia wachangie, ili tuanze ujenzi haraka, angalau tuanze na mabweni mawili ya wanafunzi wa kike halafu tutamalizia hayo mawili mengine baadaye," anasema Kalamu.

**ASASI**

Ofisa Miradi kutoka Shirika la Msichana Initiative wilaya ya Nzega, Rose Batoba alisema wamebaini kwamba kuna changamoto kubwa ya wazazi wa eneo hilo kutokuwapatia watoto wao mahitaji ya msingi, wakiaamini kwamba kutokufanya hivyo ndio njia nzuri ya kuwakatisha tamaa wasiendelee na shule ili wapate mwanya wa kuwaozesha.

"Mwamko wao wa kumpatia elimu hasa mtoto wa kike ni mdogo, wanaamini ni wa kuolewa tu, na ndio maana hawawapi mahitaji ya msingi ili watoto wakate tamaa wenyewe na waache kabisa kwenda shuleni.

"Na ndio maana sisi tuliliona hilo tukaamua kuanzisha utaratibu wa kuwasaidia baadhi ya mahitaji, zikiwamo baiskeli, madaftari na sare za shule," anasema.

Kwa mujibu takwimu za Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) mwaka 2019, miongoni mwa sababu zilizochangia wanafunzi wa kike 5,398 kukatisha masomo kwa kupata mimba ni pamoja na kutembea umbali mrefu wanapokwenda shuleni.

Air Tanzania
The Wings of Kilimanjaro

# ADVERTISEMENT

Air Tanzania Company Limited (ATCL) is expanding its network to meet the strategic business needs which focus on sustaining the recorded achievements and remain an airline of choice that meets and exceeds customers' expectations in line of its mission of provision of reliable, safe, and high-quality services. Therefore, applications are invited from qualified Tanzanians to fill the following positions: -

## 1. POSITION: SALES AND MARKETING OFFICER II (MARKETING) - (1 POST)

### 1.1 KEY RESPONSIBILITIES:

i. Develop and implement localized marketing campaigns to meet specific market trends and consumer needs.
ii. Manage regional advertising efforts, including media buys and partnerships with local channels.
iii. Collaborate with sales teams to create and execute region-specific promotions.
iv. Report on the effectiveness and outcomes of market-specific marketing activities.
v. Build and manage partnerships with local and global entities, including hotels, car rental companies, tourism boards, and more.
vi. Secure and manage sponsorship deals with sports teams, events, and other institutions to boost brand visibility.
vii. Plan and execute event marketing initiatives, ensuring Air Tanzania's presence at relevant regional events.
viii. Manage event sponsorship deals, including sporting events, conferences, and public promotions.
ix. Ensure consistent brand visibility and representation at all sponsored events and partnerships.
x. Drive brand recognition through collaboration with stakeholders and by leveraging marketing opportunities at local and global levels.

### 1.2 MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS AND WORK EXPERIENCE:

i. Must have a Bachelor's Degree in any field.
ii. Must hold one of the following certificates: Air Transport Management, Air Ticketing, Air Cargo, Dangerous Goods, Ground Handling, or equivalent qualifications from a recognized Aviation institution.
iii. Proficiency in computer applications.

## 2. TERMS AND CONDITIONS:

Ten (10) years contract for Tanzanian and with attractive remuneration and fringe benefits as per ATCL Salary Structure and Incentive Scheme.

## 3. GENERAL CONDITION FOR APPLICANTS:

i. All applications must be sent through ATCL Recruitment Portal by using the following address: https://recruitment.atcl.co.tz and NOT otherwise. This address can also be found at Air Tanzania website.
ii. Interested applicants must upload a dully signed letter for consideration of the application. The letter should be addressed to Managing Director & CEO, Air Tanzania Company Limited, P.O. Box 543, Dar es Salaam.
iii. An updated curriculum vitae (CV),
iv. Certified copies of all certificates (including secondary school, birth certificates), other relevant certificates, Applicants who have studied outside Tanzania should have their certificates approved by relevant authorities Tanzania Commission for University (TCU) or National Examination Council- NECTA)
v. Name and address of at least two reputable referees;
vi. Applicant's reliable contact address, email address and telephone number.
vii. Only shortlisted candidates will be informed on a date for interview
viii. Women are encouraged to apply.
ix. Misrepresentation of qualifications or any other information on application shall warrant legal consequences.
x. Applicants should reach the undersigned within 14 days from the first date of this announcement.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## TFF, TPLB jicho la ziada linahitajika Championship

**MPAKA** kufikia raundi ya sita ya Ligi Kuu, bado timu zilizopanda daraja, KenGold na Pamba Jiji FC, hazijapata ushindi wowote.

Pamba imecheza michezo sita, ikitoka sare minne na kupoteza miwili ikiwa nafasi ya 14, KenGold ikishika mkia, baada ya michezo yake sita ikitoka sare moja na kupoteza mitano.

Tunashangaa kuona timu hizi ambazo msimu uliopita zikiwa zinacheza Ligi ya Championship zilionekana tishio mno huku KenGold ikiongoza ligi hiyo kwa muda mrefu kabla ya kukata tiketi ya kupanda Ligi Kuu.

Ni kweli duniani kote, timu za Ligi Kuu na Ligi Daraja la Kwanza hazifanani kwa viwango, lakini havitofautiani sana mpaka kufikia hatua ya kushindwa kufurukuta zinapokutana.

Tumewahi kuona hapa hapa nchini timu kutoka Ligi ya Champioship ikipanda Ligi Kuu na kuwa tishio kwa timu ilizozikuta.

Mfano ni Azam FC iliyopanda na kuanza kucheza ligi msimu wa 2008/09, iliingia moja kwa moja na kuwa timu iliyoogopewa si na timu za Ligi Kuu tu, bali hata kwa klabu kongwe za Simba na Yanga na wala haikushangaza ilipotwaa ubingwa msimu wa 2013/14 na hadi leo inahesabiwa kuwa moja ya timu kubwa nchini.

Mtibwa Sugar, nayo ilipanda daraja mwaka 1995 na kutetemesha timu zote, kiasi cha kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara misimu miwili mfululizo 1999 na 2000.

Kama vile haitoshi, Mbeya City nayo ilipanda Ligi Kuu 2013/14, ikatokea kuwa timu hatari na ya mfano kwa timu zingine zilizokaa muda mrefu hapo.

Hiyo ni mifano ya hapa nchini tu inayoonesha kuwa viwango vya Ligi ya Championship na Ligi Kuu havipishani sana kama timu imepanda kihalali bila kutupia ujanja ujanja.

Tuna wasiwasi na baadhi ya timu za Championship zinazopanda Ligi Kuu kama kweli zinashinda kihalali, kwani katika misimu ya hivi karibuni zimetokea kuwa dhaifu sana zinapopanda kama tunavyoona KenGold ambayo iliongoza Ligi ya Championship kwa muda mrefu na Pamba Jiji ambayo iliipiku Biashara United dakika za mwisho.

Tunadhani kuna michezo michafu inayochezwa huko ikihusisha hata viongozi mbalimbali ndani ya mkoa husika katika kuhakikisha wanazipandisha timu kwa sababu za kisiasa.

Ndiyo maana tunaona karibuni kila msimu timu zinazopanda, mbili au moja ni lazima ishuke daraja, huku zinazobaki zikiponea chupuchupu.

Mfano mdogo tu, Mbeya Kwanza ilipanda na kucheza msimu mmoja tu wa 2021/22, Geita Gold ilipanda na kucheza 2023/24, lakini ikashuka, huku ikionekana kabisa kuwa haenda rekodi ikajirudia msimu huu.

Tunaona sasa ni wakati muafaka kwa Shirikisho la Soka nchini (TFF) kwa kushirikiana na Bodi ya Ligi nchini (TPLB), badala ya macho yake yote mawili kuiangalia Ligi ya Tanzania Bara, igeuze jicho moja na kulitupia Ligi ya Championship kwa manufaa ya soka la Tanzania.


Tunahitaji timu zinazopanda kuja kuleta chachu na upinzani kwenye ligi kwa ajili ya kuifanya iwe imara na izidi kupanda viwango kutoka kuwa ya sita Afrika kwenda juu zaidi.

Haiwezekani mchezaji aliyekuwa akifunga mabao kwenye Championship, ashindwe kupachika hata bao moja Ligi Kuu ikicheza na timu za madaraja ya kati tu.

Inawezekana kuwa baadhi ya timu zinapanda kiujanjaujanja na kuziba nafasi ya timu zenye uwezo ambazo zingekuja kuleta upinzani na kuwaleta usoni wachezaji wapya wenye uwezo kwa ajili ya maendeleo ya baadaye ya taifa.

Matokeo yake miaka nenda rudi wanabaki wachezaji wale wale kwenye Ligi Kuu, kwani hizi zinazopanda zilitakiwa kuja na vijana wengi wenye uwezo, badala yake asilimia kubwa zinaonekana kama hazikuwa na sifa ya wachezaji walionesha uwezo halisi na kutilia hofu huenda ulitumika ujanja ujanja tu kuzipandisha.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge

## Serikali iiangalie pia timu ya soka ya ufukweni 'BAFCON'

Na Adam Fungamwango

**OKTOBA** 19, Timu ya Taifa ya Tanzania ya soka la ufukweni itakuwa nchini Misri kupeperusha bendera ya nchi kwenye fainali za Mataifa ya Afrika za mchezo huo, BAFCON.

Watanzania wataanza kurusha karata siku hiyo watakapokipiga dhidi ya Timu ya Taifa ya Morocco.

Tanzania imepangwa kwenye Kundi A, ambalo linatajwa kuwa la kifo, lenye wenyeji Misri, Morocco na Ghana, ambapo ratiba inaonesha kuwa baada ya mchezo huo, itarejea tena uwanjani, Oktoba 21 kucheza dhidi ya wenyeji Misri, na Oktoba 22 itakutana na Timu ya Taifa ya Ghana. Kundi B lina timu za Senegal, Msumbiji, Malawi na Mauritania.

Kwa sasa timu hito kipo kwenye mazoezi makali, kabla ya kukwea pipa kwenda nchini Misri tayari kwa fainali hizo. Nahodha wa timu hiyo, Jaruph Juma, amekiri kuwa kweli wamepanga kwenye kundi gumu na akatoa sababu.

"Tumeona droo ya mashindano ya Afrika imetoka, tumebahatika kuwa kwenye Kundi A, tukiwa pamoja na wenyeji, Misri, kimsingi si kundi rahisi kama ambavyo wengine wanafikiri, na ugumu unatokana na kupangwa na mwenyeji ambaye atatumia faida ya kuwa nyumbani, pia na sisi wenyewe tunalifanya kundi liendelee kuwa gumu kwani ni wazoefu, tumeshiriki zaidi ya mara moja michuano hii, tunaamini sisi ni sehemu ya ugumu kwenye kundi," alisema.

Kwa maana hiyo, wachezaji waliounda kikosi hicho watalazimika kufanya kazi ya ziada kwa ajili ya kuliletea taifa sifa na wamehidi kufanya hivyo. Najua kuwa Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), linajitahidi sana chini ya uongozi wa rais, Wallace Karia, kwani Tanzania ni nchi pekee Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati au Afrika nzima ambayo inacheza kila michuano.

Ukisikia mashindano ya chini ya miaka 17, 20, 23, iwe ya CECAFA, au wakati mwingine COSAFA, Tanzania huwa hawakosi.

Hivyo, wakati kikosi hicho cha timu ya taifa ya soka la ufukweni kikijiandaa kuondoka, ni wajibu sasa kwa serikali kupitia Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, kuipa hamasa inayostahili na kutoa ahadi kama inavyofanya kwa mpira wa miguu wa kawaida.

Wachezaji hawa wanatakiwa waitwe, wapewe motisha, watiwe moyo ili nao wajione kuwa ni muhimu, wanathaminiwa ili waende kujituma na kupambana kwa ajili ya taifa.

Niseme tu ukiondoa Timu ya Taifa ya Wanaume, Taifa Stars, ambayo mara nyingi kabla ya kucheza michuano kama hiyo kunakuwa na hamasa kubwa, mbwembwe nyingi, lakini timu zingine, za michezo mingine, ikiwamo hata soka la ufukweni, hazipati kile ambacho wenzao wanapata.

Itakuwa si vema wachezaji wetu waondoke kimya kimya na tukasubiri mpaka wapate mafanikio ndiyo tuanze kuwaimba. Tuanze kuwaimba sasa, tutoe hamasa, serikali ikae nao na kuwaahidi ni kitu gani inaweza kuwapatia kama wakitwaa ubingwa huo.

Tanzania ina michezo mingi sana ambayo kama yote itatiliwa mkazo inaweza kupata sifa kubwa nyingi kwani baadhi ipo chini ya uwezo wao, lakini kwa bahati mbaya haitiliwi sana mkazo.

Sisemi kubwa Stars isipewe kipaumbele, lakini pia tusiisahau pia michezo mingine ambayo baadhi yao inaipa nchi umaarufu zaidi.

Mchezo wa soka la ufukweni kwa sasa umeanza kuwa maarufu na Tanzania imeanza kuonekana kuwa moja ya timu tishio barani Afrika. Inawezekana ikawa ni kwa sababu ya mazingira ya kijiografia kwani, ina fukwe za bahari, maziwa na mito, hivyo ni rahisi kimiundombinu kuliko baadhi ya nchi.

Nasikia baadhi ya nchi ambazo zinacheza michezo hiyo, zimekuwa zikichukua michanga kwa gharama kubwa kutoka kwenye nchi zilizojaaliwa na kupeleka kwao kwa ajili ya kuwezesha mchezo huo kuchezwa.

Itakuwa aibu sana kama nchi hizo zitakuwa juu ya Tanzania kwa viwango katika mchezo huo. Hivyo kinachotakiwa mbali na kusaka vipaji, mafunzo na kuiweka kambini kuitunza timu ya taifa, kuipa hamasa na kuwaahidi chochote kitu kama smbsvyo imekuwa ikifanyika kwa Taifa Stars.

## HABARI KITAIFA

# NMB 'yakazia' mafunzo ya uongozi, usimamizi jumuishi kwa wanawake

**Na Mwandishi Wetu,** KIBAHA

MAFUNZO ya Uongozi na Usimamizi Jumuishi kwa Wanawake yaliyofanyika katika Shule ya Uongozi ya Mwalimu Nyerere, Kibaha mkoani Pwani, yamefungwa Ijumaa Septemba 27, huku washiriki wakitakiwa kuweka alama chanya kwenye maisha ya wanaowaongoza, pamoja na kuwapa nafasi ya kuonesha uwezo wao.

Mafunzo hayo yaliyoshirikisha wanawake viongozi kutoka taasisi za umma na binafsi, wizara na idara za serikali, Jeshi la Ulinzi wa Wananchi Tanzania (JWTZ) na halmshauri, yalifungwa Ofisa Mkuu wa Rasilimali Watu wa Benki ya NMB, Emmanuel Akoonay, akimwakilisha Ofisa Mtendaji Mkuu, Ruth Zaipuna.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Akoonay alisema anaamini mafunzo hayo yanakwenda kuwa chachu ya kutengeneza viongozi bora zaidi miongoni mwa wanawake, na hivyo hayakuwa tu ya kuwajengea ninyi uwezo, bali pia kuongeza hamasa ya wanawake kuchangamkia nafasi za uongozi katika taasisi mbalimbali.

"Kupitia elimu mliyopata katika mafunzo haya ya wiki nzima, mmejengewa uwezo wa kukabiliana na changamoto zinazokwaza mchango wa wanawake katika ukuaji kiuchumi na uendelezaji wa taifa, tunajua mmepikwa na mmeiva tayari kwa majukumu kwenye taasisi zenu," alisema.

Akoonay alifafanua kuwa: "Dhana ya uongozi ni kuongoza wengine kufika mahali ambapo hawakuamini kama inawezekana, kwani mara nyingi inaaminika kuwa kiongozi unapaswa kuwa na dira na maono makubwa kuliko unaowaongoza.

"Na kwa sababu hiyo, ili uwe kiongozi mzuri lazima ujifunze kuweka alama chanya kwenye maisha ya wengi, hususani unaowaongoza, mjifunze kuwapa watu nafasi ya kuonesha uwezo wao, pamoja na kuongezea uwezo walionao. Ninawasihi ninyi wote mkawe aina hiyo ya viongozi huko mwendako," alisema. Alitoa wito kwa wanawake hao kuwa wasiache kujifunza na kwamba mafunzo waliyopewa yameambatana na mifano na maelezo kutoka kwa viongozi mbalimbali, wakiwamo wanawake waliopigania uhuru, ambao wameacha vitabu na machapisho ambayo yana nyongeza ya kujifunza kwao.

"Mfano hai, mimi niko chini ya kiongozi mwanamke (Zaipuna), lakini kiutendaji hatumtazami wala kumwona kama ni mwanamke, bali ni kiongozi imara, shupavu na madhubuti, ambaye tukikaa kwenye mikutano inayojumuisha wanaume wengi, sauti yake ndio inayotuunganisha na kutupa dira ya pamoja," alisema.

Naomi Mtemba aliyekuwa Mwenyekiti wa Wahitimu wa Mafunzo hayo akitokea Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ambako ni Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Ulaya na Amerika, alishukuru Serikali kwa elimu kubwa waliyopewa.

"Kwa niaba ya wahitimu, tunawashukuru walimu na wakufunzia wa shule hii, lakini pia tunashukuru Serikali ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa mpango madhubuti wa kutoa mafunzo mbalimbali ya kuwaongezea uwezo wanawake ili washiriki ngazi mbalimbali za uongozi.

"Mafunzo haya yametuwezesha kupata maarifa makubwa, ujuzi na uzoefu muhimu katika uongozi na usimamizi wa rasirimali watu, usimamizi wa majukumu yaliyo mbele yetu, usimamizi wa utekelezaji wa maelekezo mbalimbali ili kusukuma mbele gurudumu la maendeleo ya taifa na jamii," alisema.

Kaimu Mkuu wa Shule ya Uongozi ya Mwalimu Nyerere, Kabula Igambwa, alisema mafunzo hayo yalilenga maeneo mbalimbali, ukiwamo uzalendo, maslahi ya taifa, usalama, historia na harakati za ukombozi, kuongeza uwezo wa kufikiri kimkakati na misingi ya uongozi.

Aliyataja maeneo mengine kuwa ni kuongeza ujuzi binafsi wa kiongozi, watu na taasisi, kuboresha uwezo wa kubadili mawazo, kukuza utamaduni jumuishi wa taasisi, kuongeza uwezo wa kutafuta vyanzo vya rasilimali fedha na kusimamia kikamilifu miradi ya taasisi. "Pia ni mafunzo yaliyowapa nafasi ya kuongeza ujuzi wa kuongoza taasisi kimkakati, utatuzi wa migogoro, masuala ya itifaki, kufanya uamuzi bora na kujiandaa kuchukua nafasi za juu kiuongozi," alisema Igambwa katika hafla hiyo.



Wanahisa wa kampuni ya uwekezaji ya NICOL wakisoma nyaraka wakati wa mkutano mkuu wa kampuni hiyo uliofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Sheria ya Usalama Barabarani kufumuliwa

**Na Francis Godwin,** IRINGA

WIZARA ya Mambo ya Ndani ya Nchi iko katika hatua za mwisho kupeleka bungeni marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani, ambayo imesisitiza kuwa imepitwa na wakati.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchini, Daniel Sillo aliyasema hayo juzi wakati wa maadhimisho ya miaka 10 ya mabalozi wa usalama barabarani nchini yaliyofanyika kitaifa mkoani Iringa.

Alisema marekebisho ya sheria hizo yako katika hatua za mwisho kufanyiwa maboresho makubwa kisha kufikishwa bungeni ili sheria ibadilishwe na kuendana na wakati.

Naibu Waziri Sillo alisema elimu ya usalama barabarani ndiyo nyenzo muhimu kutokomeza matukio ya ajali kwa kuwa ajali hizo kwa asilimia kubwa zimeonekana zinatokana na makosa ya kibinadamu.

"Hivyo, kupitia mabalozi hao wa usalama barabarani, wanaliongeza nguvu Jeshi la Polisi na ni sawa na polisi jamii na si kuchukua nafasi za askari wa usalama barabarani," alisema.

Naibu Waziri huyo alisema kuwa mabalozi wa usalama barabarani ni sehemu ya mpango wa kitaifa uliolenga kuelimisha wananchi kuhusu mbinu bora za kuepuka ajali na kuboresha utendaji wa madereva, abiria na watumiaji barabara kwa ujumla.

"Hivyo, kupitia mabalozi hawa, elimu hutolewa kuhusu masuala kama vile umuhimu wa kuvaa mikanda ya usalama, kufuata alama za barabarani na kuepuka uendesha wa kasi," alisema.

Akielezea umuhimu wa mabalozi wa usalama barabarani, Naibu Waziri Sillo alisema kuwa hao ni watu wenye dhamira ya dhati ya kuona mabadiliko katika utamaduni wa matumizi ya barabara.

Aliwahimiza mabalozi hao kuendelea kutoa elimu kwa jamii kwa moyo ili kuokoa maisha ya watu wengi wanaopoteza maisha au kupata majeraha kutokana na ajali za barabarani.

Alipongeza wadau mbalimbali wanaojitolea kudhamini maadhimisho ya kwa miaka sita sasa, ikiwamo kampuni ya Asas kuwa mchango wa sekta binafsi ni muhimu sana katika kusaidia kampeni za serikali za kuboresha usalama barabarani.

Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mabalozi wa Usalama Barabarani (RSA) Tanzania, Augustus Fungo, alisema wamekuwa wakitoa elimu kwa jamii juu ya usalama barabarani kwa zaidi ya miaka 10, kuripoti matukio ya ajali na ukiukwaji sheria za usalama barabarani pamoja na kushawishi serikali juu mabadiliko ya sheria na sera za usalama barabarani.

Fungo aliomba serikali kuangalia upya sheria za usalama barabarani na kuzibadilisha kwa kuwa zimepitwa na wakati na kupelekea makosa ya barabarani kuendelea kuongeza kutokana na baadhi ya madereva kutokuwa na wasiwasi na sheria hizo.

"Eneo lingine linalotukwamisha ni eneo la mabadiliko la sheria za usalama barabarani, Mheshimiwa Mgeni rasmi, sheria hizi ni za zamani sana, na katika kila siku tukikutana tumekuwa tukijaribu sana kukumbishia mara kwa mara, kwamba tunahitaji kubadili sheria za barabarabi kwa sababu ni za zamani na zina faini mpaka ya Sh. 1,000," alisema Fungo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Usalama Barabarani Mkoa wa Iringa, Salim Asas alisema kampuni yake imekuwa inaunga mkono shughuli mbalimbali za kijamii kama sehemu ya jukumu lake kwa jamii na itaendelea kushirikiana na serikali katika masuala muhimu kama usalama barabarani na huduma za afya.

Alisisitiza kuwa kampuni yao inaamini katika kujenga jamii salama na yenye afya bora na ndiyo sababu wameamua kusaidia familia hizo 50 kwa bima ya afya.

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed



## Serikali yatenga mil. 100/- kujenga zahanati Saranga

**Na Beatrice Moses**

CHANGAMOTO ya ukosefu wa zahanati inayowakabili wakazi wa Mtaa wa Saranga, wilayani Ubungo, hasa wajawazito sasa inatarajiwa kuwa historia baada ya serikali kutenga Sh. 100 milioni kwa mwaka wa fedha 2024/25.

Kaimu Mganga Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Dk. John Semkuya aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa mkutano wa hadhara na wananchi wa Mtaa wa Saranga uliofanyika kwenye viwanja vya ofisi ya serikali ya mtaa huo.

Mkutano huo uliongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Hassan Bomboko ambaye alisikiliza kero mbalimbali zinazowakabili wakazi hao.

"Serikali tayari imetenga fedha hizo zinatarajiwa kushushwa ili kukamilisha jengo hilo la zahanati, ambalo lilianza kujenga kwa nguvu za wananchi," alisema Dk. Semkuya.

Awali Mweyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Saranga, Godwin Muro aliambia Nipashe kuwa amekuwa akilazimika kupisha wajawazito kuhudimiwa kwa faragha kwenye ofisi yake siku ya kliniki kwa kuwa hakuna namna, hivyo jengo hilo likikamika, itakuwa furaha na faraja kubwa kwa wananchi.

Kero nyingine zilizowasilishwa na wananchi katika mkutano huo ni pamoja na mgogoro wa mpaka kati ya Serikali ya Mtaa wa Msingwa na Saranga, hali ambayo inatajwa imesababisha Ofisi ya Mtaa wa Msingwa kujengwa Saranga.

"Nipo kwenye kamati ya urasimishaji ardhi, nilipigwa na kujeruhiwa wakati wa kazi hiyo, kwa sababu ya mpaka, jambo hili liliwahi kushughuliwa na aliyekuwa Mkuu wa Wilaya Makori, barua ya maelekezo ipo lakini hawaifuati," alisema Fred Chuku wakati akielezea kuhusu kero ya mpaka.

Kero nyingine ni ubovu wa barabara, maji kutokutoka kwenye mabomba, kuwapo vikundi vya uhalifu na kukithiri kelele za muziki katika baadhi ya maeneo nyakati za usiku, hali ambayo inawakosesha utulivu na usingizi wakazi wanaoishi karibu na majengo ya starehe.

Akijibu hoja hizo, Mkuu wa Wilaya Bomnoko aliahidi kufuatilia kwa karibu fedha hizo zipatikane kisha jengo likamilike.

Kuhusu mgogoro wa mpaka, alisema atafuatilia na kubadili matumizi ya jengo hilo la ofisi ya sasa ya Serikali ya Mtaa wa Msingwa kwa kuwa imejengwa kwa kukiuka agizo lililowekwa na mkuu wa wilaya aliyemtangulia, hivyo linapaswa kuheshimiwa.

# Madaktari JKCI watoa matibabu ya moyo kwa watoto 30 Zambia

**Na Joseph Mwendapole**

BALOZI wa Tanzania Zambia, Luteni Jenerali mstaafu Mathew Mkingule amewapongeza madaktari wanne wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) kwa kufanikiwa kuwapa matibabu mbalimbali, ukiwamo upasuaji watoto 30 wa nchi hiyo.

Madaktari hao walianza kutoa huduma hiyo ya upasuaji nchini humo Septemba 23 hadi 28 mwaka huu katika Hospitali ya Taifa ya Moyo ya nchi hiyo iliyoko mjini Lusaka.

Akizungumza wakati akiwaaga madaktari hao aliowasindikiza kwenye Uwanja wa Ndege wa Lusaka jana, Mkingule alipongeza JKCI kwa kutoa wataalamu wake ambao wamekuwa msaada mkubwa kwa wagonjwa wa moyo wa nchi hiyo.

Balozi Mkingule alisema madaktari hao na wauguzi wamefanya kazi kubwa na ya mfano nchini humo na kuahidi kuendelea kushirikiana na JKCI katika kuunga mkono uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali ya Tanzania katika sekta ya afya pamoja na kutangaza kazi kubwa na umahiri wa JKCI kwenye matibabu ya moyo.

Balozi Mkingule alitoa rai kwa hospitali zote pia kuwa na ushirikiano mzuri na nchi jirani kwa ajili ya kuendesha kambi za matibabu kama iliyofanywa na JKCI kwa kuwa wanaohitaji matibabu hayo ya kibingwa ni wengi.

Alisema Serikali ya Tanzania imefanya uwekezaji mkubwa kwenye sekta ya afya, ikiwamo kusomesha madaktari bingwa, vifaa vya teknolojia ya kisasa na ongezeko la rasilimali watu, hali ambayo imevutia wagonjwa wa nchi mbalimbali kuamua kwenda kutibiwa Tanzania.

Alisema pamoja na kuwa na huduma bora na za kisasa kama ilivyo kwa mataifa yaliyoendelea, gharama zake za matibabu ziko chini kulinganisha na mataifa mbalimbali Afrika na kwingineko duniani.

Alitoa wito kwa hospitali zote za Tanzania zenye uwezo mkubwa katika matibabu na zenye madaktari bingwa kama Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI), Hospitali ya Benjamin Mkapa, Taasisi ya Mifupa (MOI) na za binafsi kuandaa kambi za matibabu nchini humo na kuahidi kutoa ushirikiano kwa watakaokuwa tayari kufanya hivyo.

Alisema tiba utalii ni jambo kubwa duniani kwa sasa na kwamba Tanzania inatakiwa ijivunie kwa uwekezaji wake katika sekta ya afya na kuongeza kuwa wakati sasa umefika wa kuhakikisha nchi inaendelea kuwasaidia majirani katika kushirikiana nao kutoa huduma bora za afya kwa gharama nafuu na zenye mafanikio makubwa.

Aliwapongeza pia Global Medicare kwa kazi yake kubwa ya uratibu wa huduma za afya katika utalii tiba kwani mbali na matibabu wamekuwa wakiandaa taratibu mbalimbali za usafiri, mapokezi ya sehemu za kulala kwa wagonjwa, huduma za mawasiliano na bima za afya za kimataifa.

"Kambi zozote zitakazofuata, Ubalozi wa Tanzania utashirikiana na Medicare na mamlaka za hospitali za ndani ili kufanikisha kutoa elimu ya kutosha kwa umma na wahitaji wengi wa huduma hii ya afya waweze kunufaika," alisema.

Kiongozi wa ujumbe wa madaktari hao, Dk. Viviane Mlawi, alisema kuwa baada ya kumaliza matibabu hayo yeye na ujumbe wake walipata bahati ya kutembelea ofisi za Ubalozi wa Tanzania Zambia ambako walizungumza masuala mengi na Balozi Mkingule.

"Tulijadili kuhusu kambi za matibabu tumezungumza namna kambi ilivyowasaidia watoto zaidi ya 30 kupata matibabu ya moyo kwa kipindi cha kambi hii na kwa hakika imekuwa ni kambi yenye mafanikio kwani watoto wote waliofanyiwa matibabu ya upasuaji wanaendelea vizuri," alisema.




Mama Maria Nyerere (katikati), Mjane wa Baba wa Taifa, Hayati Julius Nyerere, akizungumza na msafara wa Twende Butiama 2024 ulipomtembelea nyumbani kwake Msasani, Dar es Salaam kabla ya kuanza rasmi safari ya kutoka Dar es Salaam mpaka Butiama Septemba 29 mwaka huu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Kongamano la kimataifa ubora wa elimu kufanyika Novemba

**Na Elizabeth Zaya**

KONGAMANO la Kimataifa la Ubora wa Elimu linatarajiwa kufanyika Novemba 12 hadi 14 mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Mratibu Taifa wa Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET), Martha Makala amesema kongamano hilo la elimu mwaka huu linatarajiwa kuwaleta pamoja wadau toka serikalini, watunga sera, wanazuoni, wanafunzi, walimu, watafiti, mashirika ya umma na binafsi pamoja na asasi za kiraia. Miongoni mwa mambo yanayotarajiwa kujadiliwa katika kongamano hilo ni hali ya ubora wa elimu nchini na namna unavyoweza kuendana na mabadiliko yanayoendelea duniani ya kasi ya kukua kwa teknolojia

Martha alisema jana kuwa zaidi ya wadau 300 wanaotekeleza afua za kuboresha elimu kutoka sehemu mbalimbali barani Afrika wanatarajiwa kushiriki kubadilishana mawazo, uzoefu na namna ya kutatua changamoto mbalimbali ili kuongeza tija na kuimarisha ubora wa elimu nchini. Alitaja nchi zinazotarajia kushirikia katika mkutano huo ni pamoja na Zimbabwe, Zambia, Sudani Kusini, Lesotho, Afrika Kusini, Kenya, Rwanda, Uganda pamoja na Tanzania ambayo ni mwenyeji wa mkutano huo. "Tunatarajia pia wawakilishi wa ngazi za juu kutoka Wizara za Elimu za nchi hizi kushiriki, wakiwamo mawaziri, makatibu wakuu na naibu wao na wabunge.

"Kongamano hili pia litajikita hasa katika kuleta mawasilisho na mijadala inayoendana na mwelekeo wa sera na inayolenga kutoa utatuzi wa changamoto mbalimbali za kielimu nchini na barani Afrika," alisema Martha.



## HABARI KASKAZINI



Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omari Kipanga akisalimiana na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Dk. Jumaa Mhina baada ya kuwasili Uwanja wa Jitegemee, wilayani Muheza kuzungumza na walimu katika sherehe za Juma la Elimu na uzinduzi wa kampeni ya 'Mtoto wa Leo Samia wa Kesho'. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Zainab Abdallah. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# NCAA, madiwani, viongozi wa mila, mbunge wateta

**Na Godfrey Mushi,** NGORONGORO

WAKATI serikali ikiendelea kuratibu zoezi la wananchi wa tarafa ya Ngorongoro, kuhama kwa hiari ndani ya eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), menejimenti ya mamlaka hiyo, imekutana na kufanya mazungumzo na mbunge wa jimbo hilo, madiwani kutoka kata 11 na viongozi wa mila wa jamii ya wamasai.

Kutokana na majadiliano hayo, kati ya wawakilishi hao wa wananchi na viongozi wa mila wa kimasai (Leigwanani), NCAA imelegeza sharti lililokuwa limewekwa la kuzuiwa wananchi kuingia ndani ya hifadhi hiyo kutoka saa 10:30 jioni hadi saa 12:00 jioni.

Akizungumza katika kikao hicho, Kamishna wa Uhifadhi wa NCAA, Dk. Elirehema Doriye, alisema mazungumzo hayo yalilenga kujadili masuala mbalimbali ili kuimarisha uhusiano na kutatua changamoto zilizopo ili kuimarisha shughuli za uhifadhi, utalii na maendeleo ya jamii.

"Kikao hiki ni sehemu ya NCAA kukutana na makundi mbalimbali, kwa ajili ya kuboresha uhusiano na kuainisha changamoto zilizopo, ili tuzitatue na tuendelea kuimarisha shughuli za uhifadhi, utalii na maendeleo ya jamii hasa kuboresha huduma za kijamii kwa wananchi waliopo na kuendelea kuwaelimisha kuhama kwa hiari ndani ya hifadhi," alieleza Dk. Doriye.

Aidha katika kikao hicho, Mbunge wa Ngorongoro, Emmanuel Ole Shangay, alimpongeza Doriye, kwa kuendelea kuimarisha uhusiano na wananchi wa Ngorongoro, akisema inasaidia kutatua kero za wananchi hao na kuimarisha uhifadhi shirikishi.

Ole Shangay, pamoja na mambo mengine alisema amefurahishwa na namna NCAA na Halmashauri ya Wilaya Ngorongoro, zinavyoendelea kuimarisha huduma za kijamii.

> **"Halmashauri itaendelea vilevile kukutana na wananchi kwa ajili ya kuwasikiliza, kutatua changamoto zao na kutoa elimu ya kuhama kwa hiari ndani ya hifadhi, kwa ajili kuimarisha shughuli za uhifadhi na**

"Hakuna kiongozi anayepingana na agizo la serikali kwa wananchi wa Ngorongoro, ambao wako tayari kuhama kwa hiari ndani ya hifadhi kwenda Kijiji cha Msomera (Tanga), na maeneo mengine yaliyotengwa na serikali.

"Hata yale wanayochagua wananchi wenyewe, ndiyo maana tulikuwa tunapiga kelele kwamba kuna umuhimu wa serikali kuendelea kutoa huduma kwa wananchi ambao bado hawajafanya uamuzi wa kuhama." alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro, Sadick Mbilu, alisisitiza kuwa halmashauri hiyo itaendelea kushirikiana na NCAA kuimarisha shughuli za uhifadhi na kutoa huduma za kijamii kama afya, elimu, maji na miundombinu.

"Halmashauri itaendelea vilevile kukutana na wananchi kwa ajili ya kuwasikiliza, kutatua changamoto zao na kutoa elimu ya kuhama kwa hiari ndani ya hifadhi, kwa ajili kuimarisha shughuli za uhifadhi na kuboresha maisha ya wananchi nje ya hifadhi,"alisema Mbilu.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Ngorongoro, Marekani Bayo, aliahidi kuwa baraza la madiwani litaendelea kushirikiana na NCAA katika kukuza uhusiano na kufanya uhifadhi shirikishi kupitia vijiji vyote vinavyoizunguka Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na Pori la Akiba la Pololeti.

# Watoto kuwa ma-'house girl' kwamsikitisha mbunge

**Na Oscar Assenga,** LUSHOTO

MBUNGE wa Lushoto, mkoani Tanga, Shaban Shekilindi, amesikitishwa na vitendo vya wasichana wadogo wenye umri wa kwenda shule na wenye uwezo wa kuendelea na masomo wilayani Lushoto kupelekwa mikoani kufanya kazi za ndani.

Kutokana na hali hiyo, amewataka wazazi na walezi wenye tabia hiyo ya kuruhusu watoto wao kwenda mjini kufanya kazi za ndani, kuacha na badala yake wawapeleke kusoma elimu ya sekondari ili baadae wawe msaada kwa familia.

Shekilindi alisema hayo juzi, wakati wa mahafali ya darasa la saba ya Shule ya Msingi Mkurumuzi iliyopo Kijiji cha Bombo, Kata ya Makanya, Wilayani humo.

"Sitaki kusikia tena mnawatoa watoto wanaenda mikoani kuwa house girl (wafanyakazi wa ndani). Wazazi na walezi kama mtashindwa kuwalipia ada ya sekondari, mniambie ili niweze kuwasadia kulipa gharama husika. Utaratibu ambao mtautumia ni kuhakikisha mnawasilisha majina kwa Mwenyekiti wa Kijiji au Diwani.

"Mimi nitawasaidia wanafunzi ambao hawana vifaa vya shule. Lengo letu kufika mwaka 2030, kupitia Dira ya Taifa ya Maendeleo, Kata ya Makanya iwe ina mafanikio kielimu kwa asilimia 100."

Katika hatua nyingine, mbunge huyo, alitoa onyo kwa watu wanaochonganisha wananchi na serikali, huku akieleza hatakubali kuona hilo linatokea.

Alisema: "Labda niwaambie kwamba hatukubali kuona kikundi cha watu wachache ambao wana uchu wa madaraka, kwenda kuwarubuni wananchi wa kata hii kwa sababu ya maendeleo ambayo yanatekelezwa na Rais, Samia Suluhu Hassan"

Aidha, aliwataka wananchi wa kata hiyo kuipongeza serikali kwa kuipatia Kata ya Makanya zaidi ya Sh. bilioni moja za ujenzi wa Shule ya Sekondari Bombo A.

# Samia mgeni rasmi miaka 75 Sekondari ya Umbwe

**Na Mary Mosha,** MOSHI

RAIS Samia Suluhu Hassan, anatarajiwa kuongoza wasomi na wanazuoni waliowahi kusoma Shule ya Sekondari Umbwe iliyoko Moshi Vijijini, mkoani Kilimanjaro, wakati wa Jubilei ya miaka 75 tangu kuanzishwa kwa shule hiyo kongwe nchini.

Akizungumza juzi katika uzinduzi wa kumbukizi ya kuanzishwa shule hiyo, Mwenyekiti wa wahitimu waliowahi kusoma katika shule hiyo (Alumnae), Prof. Declare Mushi, alisema Jubilei hiyo itafanyika Novemba 9 mwaka huu.

Alisema katika maandalizi ya jubilei hiyo, watajenga mnara wa kumbukumbu, kukarabati viwanja vya michezo vikiwemo vya mpira wa pete, ununuzi wa basi za shule na ununuzi wa mitambo ya umeme wa jua, utakaosaidia kuchemsha maji ya wanafunzi pamoja na matangi ya kuhifadhia maji.

"Pia tumeweka mpango wa muda mrefu wa kujenga maktaba ya kisasa kwa ajili ya wanafunzi, ambayo upande mmoja itakuwa ya kidijitali. Itafungwa kompyuta 100; na upande mwingine itakuwa ya kawaida, ambayo itakuwa na uwezo wa kuchukua zaidi ya wanafunzi 300 kwa wakati mmoja.

Alisema maktaba hiyo ya kisasa inagharimu Sh. bilioni moja, lakini hadi kufikia jubile hiyo, wanatarajia kuwa na Sh. milioni 400.

Kwa mujibu wa Prof. Mushi, wanafunzi hao wamekuwa wakiunganisha na makundi sogezi ya kila mwaka, ila kutoka na umuhimu wa tukio hilo, waliungana kwa pamoja ili kuboresha miundombinu na kukuza elimu na kuisaidia serikali katika shule hiyo.

Mkuu wa Shule hiyo, Elirehema Mungaya, akitoa taarifa kuhusu maandalizi ya kumbukizi hiyo kwa Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Raymond Mangwala, alisema shule hiyo ilianzishwa mwaka 1949.

Alisema kwa sasa shule hiyo ina wanafunzi 688 wa kidato cha tano na sita.

"Mheshimiwa Kaimu Mkuu wa Mkoa, tumekuwa tukipokea fedha kwa awamu mbalimbali kutoka serikalini kutoka mwaka 2019 hadi 2023 ambayo ni zaidi ya Sh.bilioni 1.3 kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu,"alisema.

Mmoja wa wanafunzi walioko shuleni hapo, Faraja Mosses, alisema mbali na shule hiyo kongwe kuwa na matokeo mazuri katika mitihani ya kitaifa, bado wanakabiliwa na tatizo la uhaba wa vitabu, samani katika maktaba, bwalo na mitambo ya umeme wa jua.



HABARI KANDA YA ZIWA

# Wakimbilia kwa waganga kupata matibabu ugonjwa wa kuharisha

**Na Remmy Moka,** UKEREWE

WANANCHI wilayani Ukerewe wamekumbwa na ugonjwa wa kuharisha damu, wengi wao wakiwa na imani potofu ya kwenda kutibiwa kwa waganga wa kienyeji, hali inayosababisha tatizo hilo kuendelea kuwa kubwa.

Akizungumza na Nipashe, Mratibu wa magonjwa yasiyopewa kipaumbele kutoka Hospitali ya Wilaya ya Ukerewe, Dk. Erick Mwangoka alikiri kuwepo kwa tatizo hilo na kusema kwa siku wanapokea wagonjwa 20 hadi 30 hospitalini hapo.

Alisema tatizo la kuharisha damu linatokana na usugu wa ugonjwa wa kichocho unaosababishwa na matumizi ya maji yasiyosafi na salama.

Dk. Mwangoka alisema wakazi wengi wa visiwa vya Ukerewe bado wamekumbatia imani za kishrikina wakiamini kuwa ugonjwa huo ni wakurogwa na hauna tiba za kitaalamu.

Alisema hali hiyo inasababisha kuchelewa kupata matibabu na badala yake hufika hospitalini ugonjwa ukiwa tayari umekomaa na kushindwa kupona, hatimaye wanapoteza maisha.

Hivyo, aliwataka wakazi hao kufika hospitalini mapema ili kupata hudumu ya 'Endoscopy' inayotolewa na hospitali hiyo kwa kushirikiana na madaktari bingwa kutoka Chuo Kikuu Katoliki cha Afya na Sayansi Shirikishi (CUHAS) Bugando kwa lengo la kuziba mirija ambayo inasababisha mtu kutapika na kuharisha pamoja na kuvimba miguu.

**"Kwa yeyote mwenye tatizo la namna hii nimuombe afike haraka katika Hospitali ya Wilaya ili apate matibabu, huduma hiyo tunaitoa bure ili kuwanusuru na ugonjwa huo hatari,"**

Naye Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Ukerewe, Dk. Mike Mwita alisema tatizo kubwa wananchi wengi hususani wavuvi wanatumia maji ambayo siyo safi na salama wawapo katika shughuli za uvuvi.

Alisema wananchi hao wamekuwa wakitumia maji kutoka Ziwa Victoria bila kuyachemsha hali inayosababisha kupata ugonjwa wa kichocho.

Alisema hali hiyo inawasababisha wakishindwa kwenda kupata matibabu ya kitaalam hospitalini na kwenda kwa waganga wa kienyeji, hivyo kukomaza magonjwa hayo hadi kusababisha vifo.

"Kwa yeyote mwenye tatizo la namna hii nimuombe afike haraka katika Hospitali ya Wilaya ili apate matibabu, huduma hiyo tunaitoa bure ili kuwanusuru na ugonjwa huo hatari," alisema Dk. Mwita.

Awali akizungumza na Nipashe mmoja wa wagonjwa, Alfonce Misana alisema amekuwa na tatizo hilo kwa muda mrefu hali iliiyosababisha kushindwa kutekeleza majukumu yake.

Alisema kwa sasa hali yake kiafya ni tofauti na hapo awali baada ya kupatiwa matibabu ya kitaalamu.

Vilevile alisema wakazi wengi wilayani hapo wanasumbuliwa na ugonjwa huo lakini bado hawajapata matibabu ya kina kutokana na kuamini kuwa huo siyo ugonjwa wa kawaida.



Katibu Mkuu wa ACT Wazalendo, Ado Shaibu akihutubia mkutano wa hadhara jimboni Buchosa wilaya ya Sengerema mkoa wa Mwanza juzi, ikiwa ni mwendelezo wa ziara ya viongozi ya kuimarisha chama. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wenye miaka 14 hatarini kupata homa ya ini

**Na Shaban Njia,** SHINYANGA

MRATIBU wa kuthibiti maambukizi ya ugonjwa wa homa ya ini mkoani Shinyanga, Dk. Peter Mlacha amesema vijana wenye umri kati ya miaka 14 wapo hatarini kupata maambukizi ya ugonjwa huo.

Dk. Mlacha alitaja sababu ya vijana kuwa katika hatari zaidi kuwa ni kutokana na ugonjwa huo kusababishwa na kufanya ngono zembe.

Alisema hayo juzi mkoani hapa wakati akitoa elimu ya ugonjwa wa homa ya ini kwa watumishi wa umma mkoani hapa, pamoja na mambo mengine aliyataka mashirika binafsi, umma pamoja na yasiyo ya kiserikali kuendelea kutoa elimu kwa vijana ili kuwanusuru na tatizo hilo.

Dk. Mlacha ambaye pia ni mratibu wa kuzuia maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) aliwataka wananchi kuwa na desturi ya kupima afya mara kwa mara.

Alisema kwa kufanya hivyo itawawezesha kuwa salama kwa sababu watapata chanjo na kuishi kwa usalama.

Mkazi wa Nyahanga, Denisi Kasindi alisema wananchi wengi hawana elimu ya kujikinga na ugonjwa huo ila wana elimu ya kujikinga na VVU kwa kutumia kinga na magonjwa mengine.

Alisema elimu hiyo inatakiwa kutolewa kwenye matamasha ya nyimbo za asili ambazo zimekuwa zikiwakusanya wananchi wengi.

Alisema maeneo mengine ni kwenye magulio na minada na katika mikutano ya hadhara inayofanywa na wanasiasa na itasaidia kuwafikia watu wengi kuliko inavyofanywa.

# Ofisa uchaguzi awaita wananchi kuwania uongozi

**Na Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

MSIMAMIZI wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika Halmashauri ya Buchosa mkoani Mwanza, Benson Mihayo amewataka wananchi wenye sifa ya kuwania uongozi kujitokeza kugombea katika uchaguzi huo.

Kadhalika, amewataka wananchi wenye sifa ya kupiga kura kujitokeza kutekeleza wajibu wao, ikiwa ni pamoja na kujiandikisha na kuboresha taarifa zao katika maeneo ya kata zao ili kushiriki kikamilifu katika uchaguzi huo.

Mihayo alitoa wito huo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari na kusema kuwa ushiriki wa wananchi wengi katika kugombea nafasi hizo ni muhimu katika kukuza demokrasia na kuhakikisha upatikanaji wa viongozi bora kwa maendeleo ya taifa.

Aidha, aliwataka kuwa makini na viongozi ambao wanawachagua pamoja na kuepuka kupokea rushwa kwa sababu ni kinyume na Sheria ya Uchanguzi.

"Kwa mujibu wa Kanuni ya 13 GN na 571 wakazi wote wenye umri wa miaka 18 au zaidi waliokidhi mashariti ya kisheria wanahimizwa kushiriki katika uchanguzi huu na ambao wamekamilisha miaka wanapaswa kujitokeza katika kujiandikisha na kuchukua fomu za kuwania uongozi pamoja na kushiriki kupiga kura na kugombea nafasi za uongozi," alisema Mihayo.

Aidha alisema makisio ya wananchi watakaoshiriki uchaguzi kwa Halmashauri ya Buchosa ni 221,100 na kuwa vituo 411 vitatumika katika uchaguzi huo.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda akizungumza hivi karibuni na wananchi wilayani Ilemela aliwataka kuhakikisha wanatumia vizuri tarehe za kujiandikisha katika Daftari la Mpiga Kura.

Alisema ili kuhakikisha wanatimiza wajibu wao kama wananchi wa kuwachagua viongozi wanaowataka na wenye uwezo wa kuleta maendeleo katika maeneo yao siyo vyema kukaa vijiweni na kuzunguka bila sababu za msingi, bali watumie siku hizo kujiandikisha ili kutimiza wajibu wao wa kikatiba.

Nipashe
Spotika



NYOTA WANNE WANAOWEZA KUVAA VIATU VYA RODRI CITY UK. 12-13




SZCZESNY

# MAKIPA WANNE WA KUCHUKUA NAFASI YA TER STEGEN BARCA

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA bila shaka imekuwa timu isiyo na bahati zaidi barani Ulaya linapokuja suala la majeruhi katika wiki za mwanzo za msimu wa 2024/25.

Wachezaji saba wa kikosi cha kwanza - ikiwa ni pamoja na Gavi, Ronald Araujo na Dani Olmo - wote walitolewa kuelekea mchezo dhidi ya Villarreal Jumapili, na wakati wa ushindi wa mabao 5-1 hatimaye jina lingine liliongezwa kwenye orodha ya majeruhi.

Na ilikuwa muhimu sana wakati huo. Nahodha wa klabu na kipa anayeanza Marc-Andre ter Stegen, alitolewa nje na kile ambacho kimethibitishwa kuwa jeraha la goti litakalomuweka nje hadi mwisho wa msimu.

Hapa tunawaangalia magolikipa wanne ambao wanaweza kuchukua nafasi yake, twende sasa...

**1. KEYLOR NAVAS**

Je, Keylor Navas ndiye mlinda mlango asiyethaminiwa zaidi katika kizazi chake? Ndiyo, bila shaka.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Costa Rica amekuwa na kipaji mara kwa mara kila mahali alipokuwa, na bado amebadilishwa mara kwa mara na klabu alizochezea.

Kwanza ilikuwa ya Thibaut Courtois akiwa Real Madrid na kisha, ilikuwa Gianluigi Donnarumma huko Paris Saint-Germain. Navas sasa ni mchezaji huru baada ya kuondoka PSG baada ya kumalizika kwa mkataba wake msimu wa majira ya joto, na atakuwa mbadala wa bei nafuu.

**2. WOJCIECH SZCZESNY**

Ndiyo, alistaafu soka mwishoni mwa Agosti, lakini baada ya kuandika "mwili wangu bado unahisi kuwa tayari kwa changamoto" kwenye chapisho la kijamii kuhusu kustaafu kwake, bado kuna maisha katika mbwa mzee.

Na ingawa tunasema 'mbwa mzee', katika mara ya kipa, akiwa na miaka 34, Wojciech Szczesny si mzee kihivyo.

Kipa huyo hakuonesha dalili zozote za kurudi nyuma katika miaka michache iliyopita, akitoa kiwango cha juu mara kwa mara kwa Juventus na Poland.

Sport imeripoti kwamba Szczesny anafikiria kutoka kustaafu na kuwa kipa chaguo la kwanza la Barca. Hakika anatosha kufanya kazi hiyo.

**3. GUILLAUME RESTES**

Guillaume Restes mwenye umri wa miaka 19, anaripotiwa kuwa 'anazingatiwa' kama mbadala wa Ter Stegen wakati wa dirisha la usajili la Januari.

Kinda huyo ndiye kipa chaguo la kwanza kwa sasa katika Klabu ya Toulouse ya Ligue 1, na pia katika kiwango cha Timu ya Taifa ya Ufaransa chini ya umri wa miaka 21, akicheza mechi tano hadi sasa.

Ripoti kutoka Sport inadai kuwa Barcelona watakuwa tayari kulipa ada ya euro milioni 15 pamoja na nyongeza ya euro milioni tano ili kumnasa Restes kwenda Katalunya wakati wa dirisha la usajili la Januari.

Ana uwezo wa kuchukua nafasi ya Ter Stegen kwa muda mfupi na mrefu.

**4. ALVARO VALLES**

Kipa mwingine ambaye Sport imemtaja kuwaniwa na Barca ni Alvaro Valles, kwani anaweza kuonekana kama chaguo la 'fursa ya soko' kwa 'La Blaugrana' hao.

Kutokana na mzozo wa mkataba, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, ameondolewa kwenye kikosi cha kwanza cha 'Las Palmas'. Kwa matokeo hayo, Las Palmas wanajikuta wamejikita mkiani mwa La Liga. Ambayo si bora.

Kusimama kwa mkataba kunaweza kumaanisha kuwa Barca wataweza kumnasa golikipa huyo kwa ada yenye hati punguzo.

**ISIKUPITE**

COLE Palmer amekuwa mchezaji wa kwanza kufunga mabao manne katika kipindi cha kwanza kwenye mechi ya Ligi Kuu ya England baada ya kufanya hivyo juzi, Jumamosi wakati Chelsea ikiichapa Brighton mabao 4-2. Lakini pia Palmer alifunga penalti yake ya 10 mfululizo.



## Extra Time

# NYOTA WANNE WANAOWEZA KUVAA VIATU VYA RODRI CITY



ZUBIMENDI

RODRIGO

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER City inatazamia kumkosa kiungo wao nyota Rodri kwa muda wote uliosalia wa msimu huu kutokana na majeraha mabaya aliyoyapata.

**Kiungo huyo anaonekana aliumia misuli ya paja wakati Man City walipomenyana na Arsenal kwenye Ligi Kuu England Jumapili iliyopita kwenye Uwanja wa Etihad.**

Ugonjwa wa kiungo wao bora, na mchezaji muhimu zaidi, unawaacha Man City kwenye kachumbari Christmas chungu katikati ya uwanja.

Hata hivyo, kwa bahati kwao, dirisha la usajili la Januari litawapa fursa ya kuziba pengo la Rodri.

Hapa kuna chaguzi nne bora zinazopatikana kwa kilabu hiyo dirisha hilo la Januari, twende sasa...

### Martin Zubimendi

Sawa, wacha tuondoe chaguo dhahiri zaidi kwanza. Kama alivyocheza akitokea benchi kuchukua nafasi ya Rodri kwenye fainali ya Euro 2024, Martin Zubimendi ana uwezo mkubwa wa kuziba pengo la Mhispania mwenzake katika safu ya kiungo.

Zubimendi ana uwezo huo huo adimu ambao Rodri anao, kwani ni mahiri sawa ndani na nje ya mpira - mara kwa mara akishinda zaidi ya asilimia 90 ya pambano lake na kukamilisha zaidi ya asilimia 90 za pasi zake kwa klabu ya sasa ya Real Sociedad.

Ingawa Liverpool walishindwa kumvuta kiungo huyo kutoka katika klabu yake ya utotoni msimu wa majira ya joto, nafasi ya kufanya kazi na Kocha Pep Guardiola inaweza kuwa nzuri sana kwake Januari.

### Adam Wharton

Iwapo Man City wangependelea kuangalia karibu na nyumbani kwa mchezaji ambaye wanaweza kumkuza kwa muda wa miaka michache na hatimaye kuchukua nafasi ya Rodri, basi Adam Wharton anaweza kuwa mchezaji wao.

Katika kipindi cha miezi nane iliyopita, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, aliingia uwanjani na kuwa mmoja wa wachezaji wa kati wachanga wanaozungumziwa sana barani Ulaya, shukrani kwa kiasi kikubwa kwa uwezo wake wa kudhibiti kasi ya mchezo kutoka katikati ya uwanja.

Kwa njia nyingi, mtindo wake wa uchezaji unapiga kelele 'Pep Guardiola'. Na mafunzo kidogo kutoka kwa Guardiola bila shaka yatapeleka mchezo wake kwenye kiwango cha juu.

### Ederson

Mchezaji mwingine ambaye hapo awali amekuwa akihusishwa sana na kuhamia Liverpool, Ederson amekuwa akitajwa kutaka kuondoka Atalanta kwa misimu michache iliyopita.

Na kwa kuzingatia maonesho yake huko Bergamo, ni rahisi kuona ni nini mabishano yote yamekuwa.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, amekuwa mjeruhi wa katikati ya safu ya kati ya Atalanta tangu alipong'olewa kutoka kwa Salernitana mnamo 2022, na kuruhusu wachezaji wenzake wabunifu kwenda kuchonga wapinzani bila hofu kubwa ya kuiacha timu yao juu na kavu ya kujilinda.

Labda tofauti na mchezaji mwingine yeyote kwenye orodha hii, anaweza pia kufumania nyavu kwa utaratibu sawa na Rodri - akiwa amefunga mabao mawili tu pungufu kuliko mchezaji huyo wa Kimataifa wa Hispania katika mashindano yote mnamo 2023/24.

### Morten Hjulmand

Huenda mashabiki wa England walishtushwa na kusoma jina la 'Morten Hjulmand' baada ya onesho lake la Euro 2024 dhidi ya 'Simba Watatu' hao.

Nyota huyo wa Denmark alitawala kabisa safu ya kiungo ya England wakati wa mpambano wao wa hatua ya makundi mjini Frankfurt, akimalizia mchezo mzuri kwa kufunga bao ambalo lilifanya taifa lake kutoka sare ya 1-1.

Kwenye ngazi ya klabu kwa Sporting CP, Hjulmand amekuwa mzuri sana katika miaka ya hivi karibuni pia.

Labda juu ya sifa zingine zote alizonazo, inayovutia zaidi kwa mtazamo wa Man City ni sifa zake za uongozi.

Baada ya kupata kitambaa cha unahodha wa Sporting CP baada ya msimu mmoja tu katika klabu hiyo, ni wazi kwamba Hjulmand anaweza kuingia na kuchukua nafasi ya Rodri kama kiongozi mwenye sauti katikati mwa safu ya kati ya City.

## Nukuu

"Hatukupoteza lakini ninahisi kama hasara. ulikuwa mchezo wa maisha yao, walipigania kila yadi na hatukufanya hivyo. Asilimia 99 haitoshi. Mara nyingi nadhani mtazamo wa timu hii ni mzuri sana, leo nina lawama, si timu pekee inayopaswa kujitazama kwenye kioo, mimi ni sehemu yake. Unajua tuna matatizo ya kufunga mabao, lakini lazima kuua mchezo," **Kocha wa Manchester City, Erik ten Hag, baada ya sare ya bao 1-1 dhidi ya FC Twente kwenye Europa League.**



"Nimempenda [Guardiola] tangu nikiwa na umri wa miaka 10, ninamheshimu sana. Ninashukuru sana kwa kila kitu alichonifanyia na anachoendelea kunifanyia. Iwapo mtu anataka kuharibu uhusiano, hiyo haiko mikononi mwangu. Hisia [ya mapenzi] ni kubwa. [Guardiola] anajua, wafanyakazi wanaijua kwa sababu bado [ninazungumza] nao leo, na bodi, wamiliki - na kila mtu," **Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta akikanusha kuwa na mpasuko kati yake na Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola,**



"Siwezi kukuambia [siri], je, ni Ligi Kuu tu? Kuna ligi nyingi. Nahitaji kujua ikiwa ni rekodi ya dunia au la. Lazima iwe rekodi ya dunia, michezo mitatu mfululizo chini ya sekunde 40 - haiaminiki." **Kocha wa Brentford, Thomas Frank, akizungumza na wanahabari baada ya sare ya bao 1-1 juzi dhidi ya West Ham, kuhusu timu yake kufunga bao la kuongoza sekunde ya 37, hiyo ikiwa ni mechi ya tatu mfululizo timu yake kufunga bao la kwanza ndani ya muda wa sekunde chini ya 40 kwenye mechi za Ligi Kuu England msimu huu.**






Winga wa Simba, Kibu Denis, akipambana na kipa wa Azam FC, Mohamed Mustafa, kuwania mpira uliorudishwa vibaya na mmoja wa mabeki wa timu hiyo, na kusababisha kizaazaa langoni, ingawa baadaye mwamuzi, Elly Sassi, alidai Kibu alifanya madhambi, katika Dabi ya Mzizima iliyopigwa Zanzibar wiki iliyopita. **MPIGAPICHA WETU**

# REKODI NA TAKWIMU DABI YA MZIZIMA, SIMBA, AZAM Z'BAR

**Na Adam Fungamwango**

BONGE la mechi lilichezwa Alhamisi iliyopita kwenye Uwanja wa New Amaan Complex, visiwani Zanzibar, kati ya Azam na Simba.

**Kwa sasa mechi inayozikutanisha timu hizo mbili inajulikana kama 'Mzizima Deby'. Ilikuwa ni mechi ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara, iliyomalizika kwa Simba kushinda mabao 2-0.**

Ilikuwa ni mechi ya kwanza kwa makocha wa timu zote mbili, Fadlu Davids raia wa Afrika Kusini akiwa na kikosi cha Simba, huku cha Azam kikiongozwa na Rachid Taoussi akitokea nchini Morocco.

Mara ya mwisho zilipokutana, Mei 9, mwaka huu, mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliopita, Simba ikishinda mabao 3-0, ikiwa chini ya Juma Mgunda, na Azam ilikuwa chini ya Msenegal, Youssouph Dabo.

Katika makala haya, tumekukusanyia takwimu mbalimbali za mchezo, wachezaji pamoja na rekodi za timu hizo, tukiziwasilisha kwa mtindo wa namba, twende sasa...

**47#** Dakika hii ndipo Simba alipoandika bao la pili lililowekwa kwenye kamba na Fabrice Ngoma, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, aliyeuwahi mpira uliotemwa na kipa, Mohamed Mustafa kutokana na mpira wa kichwa uliopigwa na Kibu Denis, aliyeunganisha faulo ya Jean Charls Ahoua.

**14#** Ni dakika ambayo straika wa Simba raia wa Cameroon, Christian Ateba, alifunga bao la kwanza katika mchezo huo.

Straika huyo aliwazidi mbio na nguvu, mabeki wa Azam ambao walikuwa wakimkimbiza, kabla ya kuanza kumsukuma, lakini hakuanguka ili timu yake ipate walau penalti, badala yake aligangamala na hatimaye kuukwamisha mpira wavuni.

**13#** Hii ni namba ya jezi ya mfungaji wa bao la kwanza la Simba Ateba ambaye alisajiliwa msimu huu akitokea, USM Alger ya Algeria.

**11#** Idadi hii ni ya wachezaji ambao hawakuwapo katika mchezo uliochezwa Zanzibar, lakini walicheza katika mechi ya mwisho ambayo timu hizo zilikutana Mei 9, mwaka huu.

Simba haikuwa na wachezaji sita ambao ni Ayoub Lakred, Israel Mwenda, Mzamiru Yassin, Sadio Kanoute, Freddy Michael, na Ladack Chasambi, huku Azam ikiwakosa Nathaniel Chilambo, Paschal Msindo, Yanick Bangala, Yahya Zayd na Kipre Junior.

**10#** Idadi hii ya wachezaji ndiyo iliyocheza mechi zote mbili za mzunguko wa pili msimu uliopita na ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu.

Simba ilikuwa na wachezaji wanne tu ambao walicheza pia mechi iliyopita, nao ni Mohamed Hussein 'Tshabalala', Fabrice Ngoma, Che Fondoh Malone na Edwin Balua aliyeingia kipindi cha pili, huku wa Azam ambao walicheza mechi ya mwisho msimu uliopita wakiwa ni kipa Mohamed Mustafa, Yeison Fuentes, Feisal Salum, Gibril Sillah, James Akaminko, na Idd Selemani Nado.

**6#** Namba ya jezi ya kiungo wa Simba, Fabrice Ngoma, aliyefunga bao la pili katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Azam, Alhamisi iliyopita, Uwanja wa New Amaan, Zanzibar.

**5#** Jumla ya wachezaji sita wa Simba waliugusa mpira kabla ya bao la kwanza dhidi ya Azam FC kuingia nyavuni. Ulianzia kwa Moussa Camara, akampelekea pembeni kidogo, Fondoh Che Malone, ambaye aliurudisha ndani kidogo kwa Abdulrazack Hamza, naye aliupeleka mbele kwa Joshua Mulate, ambaye alimsogezea Jean Charles Ahoua, akapiga pasi ya juu pembeni winga ya kulia ambayo ilimkuta mfungaji, Ateba aliyeanza safari ya kwenda kuuweka wavuni.

**2#** Namba hii inasimama kwa Ngoma ambaye ni mara ya pili mfululizo kufunga bao dhidi ya Azam FC.

Alifanya hivyo Ligi Kuu msimu uliopita, Mei 9, mwaka huu, Uwanja wa Benjamin Mkapa, ikiwa ni mechi ya mzunguko wa pili. Mechi zote hizo alifunga mabao ya pili kipindi cha pili.

Alifunga bao la pili dakika ya 77, kwenye ushindi wa mabao 3-0, mengine yakiwekwa wavuni na Sadio Kanoute na David Kameta. Katika mchezo uliopita, alifunga tena bao la pili katika ushindi wa mabao 2-0 mjini Zanzibar.

**1#** Ni mara ya kwanza kwa mechi ya Dabi za Mzizima ya Ligi Kuu Tanzania Bara, kuchezwa kwenye Uwanja wa New Amaan Complex, Zanzibar.

**0#** Azam haijapata bao lolote katika michezo miwili ya Ligi Kuu Tanzania Bara ikicheza dhidi ya Simba. Alhamisi iliyopita ilichapwa mabao 2-0 katika mchezo wa mzunguko wa kwanza, na mechi ya mzunguko wa pili msimu uliopita, Mei 9, mwaka huu, haikuambulia kitu, ikifungwa mabao 3-0.

**JE, WAJUA?**



BRENTFORD inaaminika inaweza ikawa imeweka rekodi ya dunia kwa kufunga bao la kwanza chini ya sekunde 40 katika mechi tatu mfululizo za Ligi Kuu England; ilianza Septemba 14, dhidi ya Manchester City, ambapo Yoann Wissa aliingia kambani sekunde ya 22 tu tangu mechi ilipoanza, kisha Septemba 21 dhidi ya Tottenham, Bryan Mbeumo akaziona nyavu sekunde ya 23 na juzi Jumamosi Septemba 28, Mbeumo tena akatupia bao sekunde ya 37 dhidi ya West Ham.





## Watoa mapendekezo namna kudhibiti taka za plastiki

**Na Halfani Chusi**

WADAU wa mazingira nchini kwa kushirikiana na taasisi za kimataifa wametoa mapendekezo kuhusu majadiliano ya mkataba wa kuzuia taka za plastiki duniani ili uwe na tija na kumaliza tatizo la uchafuzi wa mazingira.

Katika mkutano huo Tanzania itawakilishwa na maofisa kutoka Balaza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkurugenzi wa taasisi ya Nipe Fagio ambayo inajihusisha na utunzaji wa mazingira, Anna Rocha aliwashauri viongozi watakaokwenda katika majadiliano ya mkataba huo kuzingatia mambo kadhaa ikiwamo kulinda afya, mazingira na haki za binadamu.

Alisema lazima watoe mkataba unaofaa kwa lengo la kumaliza uchafuzi wa plastiki na ulingane na maagizo ya UNEA 5/14.

"Plastiki ni janga linalokuwa kwa kasi likiwa na athari kubwa kwenye mazingira, afya ya binadamu, haki za binadamu, haki ya kimazingira, haki za watu wenyeji katika eneo husika, viumbe hai na hali ya hewa" alisema Anna.

Anna alisema kunatakiwa kuwapo na hatua za pamoja za kidunia za haraka kupambana na janga hilo.

Alisema mkataba huo unapaswa uwe na malengo ya lazima ya kuzuia na kupunguza vyanzo vya uzalishaji wa plastiki, kupunguza kiwango cha janga la uchafuzi utokanao na plastiki.

Vilevile alivitaja vipengele muhimu ambavyo vinapaswa kuzingatiwa kuwa ni pamoja na kupunguza uzalishaji wa plastiki kwenye chanzo, sheria na malengo ya kisheria juu ya uzalishaji na usambazaji wa plastiki mpya, uzuie kemikali hatari kwa afya ya binadamu na mazingira.

Alisema pia unapaswa utoe sheria maalum zinazotekeleza kanuni za tahadhari na kanuni za "hakuna data, hakuna soko" ili kuondoa vikundi vya kemikali vinavyohatarisha afya ya binadamu na mazingira. Alisema ahadi za kisheria za kumaliza uchafuzi wa plastiki zinapaswa kuendana na ahadi za wazi za kutoa fedha kimataifa.

"Vilevile, tunapaswa kuepuka mtazamo wa fedha za hiari kwa hatua za hiari ambao umeshindwa katika makubaliano mengine" alisema.

Alisisitiza mkataba huo lazima uhakikishe mpito wa haki kwa wakusanya taka walio mstari wa mbele, jamii zingine zinazoathirika moja kwa moja na athari za plastiki.

Kadhalika, alisistiza hiyo inajumuisha msaada wa kifedha, kutambuliwa rasmi kwa haki zao, uwazi juu ya athari za kiafya za uchafuzi wa plastiki na ushiriki kamili katika utungaji sera.

# Hukumu kesi ya 'waliotumwa na afande' kutolewa leo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KESI ya jinai ya kubaka na kumwingilia kinyume cha maumbile mkazi wa Yombo Dovya jijini Dar es saalam (jina limehifadhiwa), inatarajiwa kutolewa hukumu leo na Mahakama ya Hakimu Mkazi Dodoma.

Kesi hiyo Namba 23476 ya Mwaka 2024 inawakabili washtakiwa wanne wakiwamo askari wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), MT 140105, Clinton Damas, askari magereza C.1693 Praygod Mushi, Nickson Jackson na Amin Lema.

Akizungumza na waandishi wa habari Septemba 27 mwaka huu, wakili wa washtakiwa hao, Meshack Ngamando alisema kila kitu kilichotakiwa kwenye kesi hiyo kimekamilika, kinachosubiriwa sasa ni uamuzi wa mahakama.

Alisema mwishoni mwa wiki walifanya mawasilisho ya mwisho ya kisheria kuhusu mwenendo wa kesi hiyo na kwamba wamewasilisha hoja kuhusu kasoro zilizojitokeza wakati wa usikilizaji.

**"Tumepata nafasi ya kuwasilisha mawasilisho ya mwisho, kuhusu mwenendo wote wa kesi kuanzia hati ya mashtaka, ukamataji, utambuzi, mashahidi, vielelezo vilivyotolewa mahakamani"**

"Tumepata nafasi ya kuwasilisha mawasilisho ya mwisho, kuhusu mwenendo wote wa kesi kuanzia hati ya mashtaka, ukamataji, utambuzi, mashahidi, vielelezo vilivyotolewa mahakamani kwa muda wa saa tatu na upande wa serikali nao umewasilisha yao kuanzia saa 11.00 jioni hadi saa moja usiku kwa hiyo kinachosubiriwa kwa sasa ni uamuzi wa mahakama," alisema Ngamando.

Alisema mwenendo wa kesi ulikuwa mzuri na kumbukumbu zilichukuliwa vizuri.

Wakili Godfrey Wasonga alisema wapo tayari kwa uamuzi utakaotolewa na mahakama.

Utetezi wa washtakiwa hao ulifungwa Septemba 26, 2024 ambao ulitolewa na washtakiwa pekee na hakukuwa na kielelezo chochote.



Diwani wa Ipagala, Ngombo Dotto akizungumza na wahitimu wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Makole, jijini Dodoma (hawapo pichani) wakati wa mahafali ya 15 yaliyofanyika juzi. Kushoto ni Mkuu wa shule hiyo, Beatrice Mangole. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Punda, mbwa waondolewa orodha wanyama wanaoliwa

**Na Thobias Mwanakatwe,** DODOMA

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imefanya maboresho ya kanuni kwa kuwaondoa punda na mbwa katika orodha ya wanyama wanaotakiwa kuchinjwa na kufanywa kitoweo.

Naibu Mkurugenzi wa Haki za Wanyama na Ustawi wa Wanyama, Dk. Annette Kitambi, alisema hayo juzi wakati wa warsha ya wadau iliyolenga uwasilishaji wa tathimini ya ustawi wa wanyama.

Alisema marekebisho ya kanuni hiyo yatasaidia kumlinda mnyama punda ambaye katika baadhi ya mikoa imekuwa ikimchinja mnyama huyo na kufanywa kitoweo, jambo ambalo linahatarisha kutoweka.

Dk. Kitambi alisema hatua nyingine zinazochukuliwa na serikali ni kufanya marekebisho kwenye mitaala ya mafunzo, ili baadhi ya wanyama akiwamo punda waweze kutajwa vizuri na hivyo wasiweze kupotea nchini.

"Katika kuhakikisha punda wanakuwa wengi nchini, tumeona kuna umuhimu wa kufanya utafiti wa uzalianaji wa punda maana inawezekana tatizo la punda kutozaliana kwa wingi linazababishwa na matunzo duni anayopewa," alisema.

Dk.Kitambi alisema pia serikali imekuwa ikitoa elimu ya ustawi wa mnyama punda kwenye minada, luninga na redio, uteuzi wa wakaguzi wa masuala ya ustawi wa wanyama katika mamlaka za serikali za nitaa na uteuzi wa bodi ya kumshauri waziri masuala ya ustawi wa wanyama nchini.

Daktari wa mifugo kutoka sekta binafsi, Dk.Bedan Masuruli, akiwasilisha ripoti ya tathimini ya hali mnyama punda, alisema licha ya katazo la serikali lililotolewa 2021 lakini bado biashara ya mnyama huyo inaendelea kufanyika hapa nchini.

Dk. Masuruli alisema hivi sasa punda wengi kutoka mikoa mbalimbali wanasafirishwa kupelekwa Mkoa wa Geita lakini bado haijafahamika wakifikishwa katika mkoa huo wanapelekwa wapi.

Alisema hata biashara ya ngozi ya punda bado inafanyika kwa kasi sambamba na kusafirishwa kutoka Tanzania Kwenda Kenya. Alisema kuna haja kwa Serikali ya Tanzania ishirikiane na Serikali ya Kenya katika kudhibiti biashara ya punda.

Mkurugenzi wa Shirika la Inades Formation Tanzania (IFTz), Mbarwa Kivuyo, alisema shirika hilo kwa kushirikiana na Brooker East Africa wamekuwa mstari wa mbele kuhakikisha haki na ustawi wa mnyama punda analindwa.

# Wakulima watakiwa kujiepusha na sumukuvu

**Na Mwandishi Wetu**

WAKULIMA kutoka kata 15 kati ya 40 wilayani Kilosa mkoani Morogoro zinazozalisha mahindi na karanga kwa wingi wametakiwa kujiepusha na sumukuvu kwenye mazao ili kulinda afya za walaji.

Akizungumza na wakulima hao, Ofisa Udhibiti Ubora kutoka Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Gerald Magola, alisema walikuwa wilayani humo kutoa mafunzo kwa wananchi namna ya kupambana na sumukuvu.

Magola alisema sumukuvu kwenye mazao hayo ndiyo imeripotiwa kuwa ni hatari zaidi kuliko nyingine ambazo zinapatikana katika mazao mengine.

Alisema kwa mwaka huu elimu imeshatolewa katika mikoa mitatu ambayo ni Simiyu, Tabora na Morogoro. Ofisa Udhibiti Ubora kutoka TBS, Kaiza Kilango, alisema njia ya kuondoa sumukuvu ni wakulima kuzingatia kanuni bora za kilimo kwa kuandaa mashamba yao kwa wakati, kupanda mbegu bora, kulima mazao yao kwa wakati.

Pia, kutumia mbolea, kuvuna kwa wakati, kuvuna kwa kuzingatia ushauri wa kitaalam, mazao yanapovunwa yasianikwe chini kwa sababu fangasi wanakuwa chini kwenye udogo.

Aidha aliwataka wakulima hao kuhakikisha wanaanika kwenye maturubai au vichanja nafaka zao mahindi au karanga pindi wanapofika nyumbani.

Pia, aliwataka kupukuchulia `kwa mashine ambazo hazitaruhusu kuvunjika kwa mahindi, kwani yanapovunjika yanasababisha fangasi wa sumukuvu kushambulia mahindi kirahisi.

Alisema mahindi hayatakiwi kuwekwa kwenye sakafu ili kuzuia unyevunyevu ili kuruhusu mzunguko mzuri wa hewa na alishauri mahindi yachambuliwe ili kuondoa ambayo yameonesha dalili ya kushambuliwa na sumukuvu.



# Vijana watakiwa kupuuza taarifa potofu kuhusu BBT

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa amewataka vijana kuacha kusikiliza maneno ya upotoshaji kuhusu mradi wa BBT ulioanzishwa wilayani humo.

Amesema nia ya serikali ni njema ya kuhakikisha vijana wanaingia kwenye kilimo ili kupata kipato kitakachosaidia kuinua hali zao kiuchumi.

Alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa mkutano wenye lengo la kutoa mrejesho juu ya mradi huo ambao ulianzishwa wilayani Njombe ili vijana watumie fursa hiyo.

Kissah alisema kunapokuwa na jambo zuri lazima kuna watu ambao hawana nia njema na hawapendi kuona serikali inafanikiwa katika kuwasaidia vijana na makundi maalum.

Alisema watu wa aina hiyo wanapenda kuona vijana wanakuwa walalamikaji katika nchi yao ambayo imewapa fursa nyingi ikiwemo kilimo.

"Kwahiyo wasisikilize maneno ya wapotoshaji tuweze kwenda mbele tushikilie lengo letu ambalo limetuleta kuanzisha hii BBT katika wilaya yetu," alisema.

Alibainisha kwamba vijana ambao wameomba mikopo kwa ajili ya kufanya kilimo watumie vizuri fedha watakazopata kwa malengo yaliyokusudiwa ili tija iweze kupatikana.

Alisema tayari Wizara ya Kilimo imetoa matrekta matano kwa Wilaya ya Njombe kwa ajili ya kutekeleza mradi huo kwa vijana pamoja na ekari 500 zimetengwa Halmashauri ya Mji wa Njombe ili kutekeleza mradi huo kwa vijana zaidi ya 2000.

**"Kwahiyo wasisikilize maneno ya wapotoshaji tuweze kwenda mbele tushikilie lengo letu ambalo limetuleta kuanzisha hii BBT katika wilaya yetu," alisema.**

Mkurugenzi Mtendaji Mfuko wa Pembejeo (AGITF), Mwanahiba Mzee alisema lengo la kuanzishwa kwa mfuko huo ni kuhudumia wananchi pale ambapo taasisi za fedha hazifiki.

Mratibu wa BBT kutoka Wizara ya Kilimo, Vumilia Zikankaba alisema lengo la kuanzishwa kwa mradi huo ni kuwasaidia vijana kwenda kwenye kilimo ili kutatua changamoto ya ajira nchini.

"Mradi huu ni watofauti kwani umeangalia matatizo ambaye yalikuwa hayatatuliki muda mrefu na yanayosababisha kijana wasiingie kwenye kilimo," alisema Zikankaba.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Njombe, Erasto Mpete aliwataka vijana kuchangamkia fursa hiyo ya kilimo kupitia mradi huo ili waweze kujiimarisha kiuchumi.

Mmoja ya kijana ambaye ni mnufaika wa mradi huo wilayani Njombe, Yuda Gulty alisema Mei mwaka huu walielezwa kuhusu fursa hiyo na namna itakavyowanufaisha baada ya utekelezaji wake.

Alisema vijana wengi walijaza fomu kwa ajili ya kuomba mikopo ya kilimo lakini baadhi walifanikiwa na wengine walishindwa kutokana na kutokidhi vigezo.




Mkuu wa Hifadhi ya Taifa Ruaha, Godwel Meing'ataki akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) mkoani Iringa jana kuhusu maadhimidho ya miaka 60 ya hifadhi hiyo yatakayofanyika Oktoba 1-7 mwaka huu. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Ugonjwa kichaa cha mbwa waua watu 1,500

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WATU 60,000 wanafariki dunia kila mwaka duniani kutokana na ugonjwa wa kichaa cha mbwa, huku Tanzania watu 1,500 wanafariki kutokana na ugonjwa huo.

Hayo yalielezwa mwishoni mwa wiki na Ofisa Mfawidhi wa Kituo cha Udhibiti wa Magonjwa ya Wanyama Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Dk. Jeremia Chonga katika maadhimisho ya Siku ya Kichaa cha Mbwa Duniani ambayo yalifanyika Mtaa wa Sigridi katika Halmashauri ya Mji wa Makambako wilayani Njombe.

"Takwimu zinaonesha Tanzania pekee zaidi ya watu 1,500 kila mwaka wanafariki dunia kwa sababu ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa," alisema Dk. Choga.

Ofisa Kilimo, Mifugo na Uvuvi kutoka Halmashauri ya Mji wa Makambako, Beatrice Tarimo alisema wafugaji wa mbwa wanapaswa kuzingatia kanuni bora za ufugaji kwa kuhakikisha wanatoa chakula bora na matibabu.

"Halmashauri itaendesha zoezi la kutoa chanjo ya kichaa cha mbwa kwa mwezi mmoja kuanzia Septemba 28 hadi Oktoba 28 mwaka huu katika mitaa na vijiji vyote," alisema Tarimo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Makambako, Hanana Mfikwa aliwataka wananchi ambao wamefuga mbwa na paka kuhakikisha wanapatiwa chanjo ya ugonjwa huo ili kuepuka athari zinazoweza kujitokeza.

Baadhi ya wananchi mjini Makambako akiwemo, Pascal Chengula alisema bado elimu inatakiwa kutolewa kwani wafugaji wengi wanafuga mbwa bila kujua kanuni bora za ufugaji na kusababisha washindwe kuwahudumia kwa kutowapatia chakula bora, matibabu na malazi.

Fransisca kigumu alisema ipo haja ya serikali kuanza kuwachukulia hatua za kisheria wafugaji wote ambao wanafuga mbwa na wanashindwa kuwahudumia.

Alisema hali hiyo inasababisha adha kwenye jamii kutokana na mbwa hao kuzurula mtaani na kutishia usalama wa watoto na kukamata kuku.

Kauli mbiu ya maadhimisho hayo inasema 'Ondoaa vizingiti vinavyokwamisha mapambano dhidi ya kichaa cha mbwa'.

Katika maadhimisho hayo Halmashauri ya Mji wa Makambako imeweka mpango wa kuchanja mbwa 6,000 na paka 500 kwa kipindi cha mwezi mmoja kuanzia Septemba 28 hadi Oktoba 28 mwaka huu.

# Vituo 121 kutumika kuandikisha wapigakura Njombe

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

HALMASHAURI ya Mji wa Makambako mkoani Njombe, imetenga vituo 121 kwa ajili ya wananchi wenye sifa ya kushiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa kujiorodhesha kwenye Daftari la Mpiga Kura kuanzia Oktoba 11 hadi 20 mwaka huu.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki na msimamizi wa uchaguzi ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Makambako, Kenneth Haule wakati akitoa maelekezo ya uchaguzi kwa wadau mbalimbali wa uchaguzi wakiwemo viongozi wa vyama vya kisiasa, dini na wawakilishi wa wafanyabiashara na madereva bodaboda.

Alisema zoezi la kujiandikisha kwenye daftari hilo litadumu kwa siku 10 na kila mtaa na kitongoji utakuwa na kituo.

"Wananchi wote wenye sifa ya kushiriki uchaguzi wanatakiwa kujiorodhesha kwenye Daftari la Mpiga Kura ili wapate fursa ya kuchagua viongozi wanaowataka pia nawasisitiza wadau kwenda kutoa elimu kwa wananchi ili kushiriki zoezi hili," alisema Haule.

Aidha, alisema kila mwananchi mwenye sifa anatakiwa kujiandikisha kwenye mtaa ama kitongoji anacho ishi badala ya maeneo ambayo wanafanyia shughuli za kiuchumi.

Nao viongozi wa kisiasa akiwemo Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Wilaya ya Njombe, Seth Vegula alisema atahakikisha anatoa elimu kwa wananchi ili wajiandikishe kwenye Daftari la Mpiga Kura ili wapate nafasi ya kuchagua viongozi wanaowataka.

Katibu wa Siasa, Mafunzo na Uenezi Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Njombe, Hitra Msola alisema: "Tutahakikisha tunatoa elimu kwa wananchi ili wajiandikishe na wapate fursa ya kuchagua viongozi wanaowataka kwenye uchaguzi huu".

Kwa upande wao viongozi wa dini akiwemo, Shekhe Ibrahim Chang'a aliwataka viongozi wa siasa na wasimamizi wa uchaguzi kutanguliza mbele maslahi ya taifa kwa kusimamia haki na kutumia maneno ya kudumisha amani badala ya kuhamasisha uvunjifu wa amani.



# Idadi wageni wanaoingia Zanzibar yaongezeka

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

IDADI ya wageni wanaoingia Zanzibar kipindi cha Agosti mwaka huu imeongezeka kutoka 61,466 waliongia kipindi kama hicho mwaka jana hadi 72,296 mwaka huu.

Mkuu wa Diveshini ya Utoaji Huduma, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Bakar Khamis Kondo, alisema hayo juzi wakati akiwasilisha takwimu hizo.

Alisema ukilinganisha na wageni 68,223 walioingia Julai 2024 ni ongezeko la asilimia 6.0, kwamba alitaja Italia ndiyo iliyongoza kwa kuleta wageni 12,367 (17.1%) ya wageni wote ikifuatiwa na Ufaransa iliyokuwa na 6,228 (8.6%).

Alisema Ujerumani imeshinda namba tatu kwa kuingiza wageni 5,131 (7.1%), huku Uingereza ikishika nafasi ya nne kwa kuingiza wageni 4,671 (6.5%) na ya tano ilikuwa Poland iliyoingiza wageni 3,389 (4.7%).

Kondo alisema wageni 48, 879 waliingia nchini kutoka Bara la Ulaya (67.6%), huku Bara la Afrika likifuatia kwa kuwa na wageni 10,321 (14.3%) ya wageni wote waliongia Agosti, 2024.

Aidha alisema Bara la Asia lilikuwa la tatu kwa kuwa na wageni 7,700 (10.7%) na Oceania lilikuwa na wageni 788 (1.1%).

Alisema wageni 61,748 (85.4%) waliingia Zanzibar kupitia katika viwanja vya ndege na wageni 10,548 (14.6%) waliingia kupitia Bandarini.

Hata hivyo, alisema asilimia 99.3 ya wageni walikuja nchini kwa ajili ya mapumziko, huku asilimia 0.5 kuwatembelea ndugu na marafiki na asilimia 0.2 waliingia kwa ajili ya sababu mbalimbali kama vile biashara na mikutano.

Naye Ofisa Takwimu kutoka Kamisheni ya Utalii Zanzibar (ZCT), Maabad Jaffar Muhiddin, alisema wataendelea kushirikiana na wadau ndani na nje ya nchi katika kuimarisha sekta ya utalii nchini.

Alisema Zanzibar bado ina fursa nyingi ambazo zikitumika vizuri zinaweza kuongeza idadi ya watalii ikiwemo michezo ya kiutalii na makongamano ya kimataifa.

Mtakwimu kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BoT) Tawi la Zanzibar, Paul Lawuo, alisema kutokana na kukuwa kwa sekta ya utalii, uchumi wa nchi unaendelea kuimarika na hali ya wananchi inabakia kwenye njia sahihi.

Ofisa Uhusiano Idara ya Uhamiaji Zanzibar, Shariff Bakar Shariff, alisema idara hiyo imeimarisha huduma zake ikiwemo mifumo ya kielektroniki kwa kuwawezesha wananchi na wageni kuomba visa kwa urahisi zaidi.

Mjumbe Jumuiya ya Kampuni ya Watembeza Watalii Zanzibar (ZATO), Thabit Abdurazak Abdurahman, aliishauri serikali kuendelea kuimarisha usalama wa wageni ili kuiweka sekta hiyo katika ufanisi.

# Dk. Mwinyi awapa maagizo UVCCM kuelekea uchaguzi

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amewataka UVCCM kuweka mikakati maalum ya kuhakikisha wanachama wa chama hicho wanajiandikisha ili washiriki uchaguzi mkuu ujao.

Alitoa rai hiyo juzi Mkoa wa Kusini Unguja kwenye mahafali ya wanafunzi wa vyuo na vyuo vikuu Zanzibar, yaliyoandaliwa na UVCCM.

Pia, aliutaka umoja huo kuhakikisha wanachama wao wote wanajiandikisha kwenye Daftari la Mpiga Kura ifikapo Januari 2025.

Kadhalika, aliwataka vijana kuendelea kuwa raia wema, wenye nidhamu na uzalendo pamoja na kufuata malezi na mustakabali mwema.

Pia, aliwaahidi viongozi na wanachama wa UVCCM kwamba serikali itaendelea kuchukua hatua za kuzitafutia ufumbuzi changamoto mbalimbali zinazowakabili kwa kuwashirikisha katika masuala ya maendeleo ikiwemo uongozi.

Hata hivyo alisema Serikali ya Zanzibar imeongeza bajeti ya sekta ya elimu ili kuwawezesha vijana kunufaika na mikopo na kuendelea na elimu ya juu.

**Kadhalika, aliwataka vijana kuendelea kuwa raia wema, wenye nidhamu na uzalendo pamoja na kufuata malezi na mustakabali mwema.**

Alisema serikali imeongeza bajeti ya elimu kutoka sh. bilioni 265.5 kwa mwaka 2021/2022 na kufikia Sh. bilioni 851 mwaka 2024/2025.

Vilevile, aliwahakikishia vijana wote wanaopata fursa ya kujiunga na elimu ya juu kuwa watapata mikopo isiyo na masharti na kueleza, kwamba serikali imeongeza bajeti ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Zanzibar kutoka Sh. bilioni 4.0 mwaka 2011 hadi Sh. bilioni 33.50 mwaka 2024.

Alisema kiwango hicho cha fedha kinawasomeshea vijana 7,367 wa elimu ya juu kwa kuwanufaisha wanaosoma vyuo vya ndani na nje ya nchi.

Dk. Mwinyi alisema ili kuhakikisha vijana wengi zaidi wananufaika na fedha hizo, tayari serikali imeanza kutoa mikopo kwa wanafunzi wanaosoma ngazi za stashahada.

Alisema wanafunzi 365 wenye ufaulu bora zaidi wa daraja la kwanza wananufaika na ufadhili unaotolewa na serikali kwa kushirikiana na wadau.



Mwenyekiti wa ACT Wazalendo, Othman Masoud akihutubia mkutano wa hadhara wa chama hicho Konde kisiwani Pemba mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vitalu vya mafuta na gesi asili vyatangazwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi imetangaza vitalu vya mafuta na gesi asili vya nchi kavu, kwamba hatua hiyo imefikiwa baada ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na taasisi zake zinazosimamia sekta hiyo kukamilisha tathmini.

Akizungumza na waandishi wa habari, Waziri wa Wizara hiyo, Othman Shabani, alisema baada ya kitalu hicho kurejeshwa serikalini na kampuni ya AKGAS kumaliza muda wa leseni yake, eneo hilo limegaiwa katika vitalu viwili.

Alivitaja vitalu hivyo ni Z1 chenye ukubwa wa kilomita za mraba 6,572 na Z2 chenye ukubwa wa kilomita 6,242.

Alisema vitalu hivyo sasa viko wazi kwa uwekezaji na kampuni za kimataifa za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia zinakaribishwa kuwasilisha mapendekezo yao, ili kufanya majadiliano na serikali, kisha kuingia mikataba.

Othman alisema uamuzi wa kuvitoa vitalu hivyo kwa njia ya majadiliano unaenda sambamba na dira ya kimkakati ya serikali ya Zanzibar ya kuvutia uwekezaji katika shughuli za mafuta na gesi asilia kwa lengo la kuendeleza rasilimali hizo kwa njia endelevu.

Aidha, alizitaka kampuni za kimataifa za mafuta na gesi asilia kutumia fursa hiyo kuwekeza Zanzibar katika sekta hiyo.

Akitoa mrejesho kuhusu duru ya kwanza ya utoaji wa vitalu vya Zanzibar iliyozinduliwa Machi 20 mwaka huu kwa vitalu vinane vya baharini, alisema baada ya kuzinduliwa serikali imefanya kampeni kubwa ya kuvitangaza ili kuzivutia kampuni za kimataifa za mafuta na gesi asilia kushiriki katika duru hiyo.

Hata hivyo, alisema katika jitihada ya kuvitangaza vitalu hivyo na kuvutia wawekezaji, serikali imeshiriki katika mikutano mitatu ya kimataifa ya sekta ya mafuta na gesi asilia.

Alisema mikutano hiyo ilifanyika, Uingereza, Norway na Marekani na Serikali ya Zanzibar kupitia Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi imepanga kuendelea kuvitangaza vitalu nane vya duru ya kwanza katika mikutano miwili ya kimataifa itakayofanyika Oktoba na Novemba mwaka huu Afrika ya Kusini kwa lengo la kuvutia wawekezaji.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**MASANZU JUMA ATHUMANI** anatangaza kupotea kwa kadi ya Bajaji yenye namba za usajili MC 921 CPK. Chassis namba MD6M14PA5L4C07190. Engine namba AK4CL4407013. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/208742/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BABY MARIEBAKHITA KAMBINDA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 609 DUQ - BMW**. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/207447/2024.**

---

**FOMU MIRATHI - 2**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Shauri la Mirathi Na. 1550/2024**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU**
**HASINA ELIFURAHA MANENTO WA.................**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA**
**AMIRI RAMADHANI MANENTO**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 16 mwezi 10 mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.
Imetokewa leo tarehe 27 mwezi 09 mwaka 2024.

HAKIMU

## KUPOTEA KWA VYETI



**ATOSHAEL MOSES LAIZER** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0194/0080 kilichotolewa na FARAJA SEMINARY mwaka 2018. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba S1757/0559 kilichotolewa na BENDEL MEMORIAL mwaka 2021. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DOD/DOD/31674/2024.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MBEYA**
**SHAURI LA UKAZAJI HUKUMU NA 20159 / 2024**
**(ILIPOANZIA KWENYE KESI YA MADAI NA 46 OF 2019)**
**TATA AFRICA HOLDINGS (TANZANIA LTD)...................MDAI**
**DHIDI YA**
**EZEKIEL ALLAN MWAIGAGA...............MDAIWA**

**KWA: EZEKIEL ALLAN MWAIGAGA**
**POPOTE ULIPO.**

Kwa kuwa mdai ameleta madai ameleta maombi ya ukazaji hukumu mnamo tarehe 30/08/2024. Hivyo unaamriwa kufika mbele ya Mahakama hii wewe mwenyewe au Wakili wako, mnamo tarehe 2/10/2024 saa mbili na nusu asubuhi bila kukosa.

Elewa kwamba ukikosa kufika siku hiyo shauri hilo litasikilizwa upande mmoja bila wewe kuwepo, na uamuzi utatolewa upande mmoja.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu pamoja na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 17/09/2024.

HAKIMU MKAZI
SENIOR RESIDENT MAGISTRATE MBEYA
MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MBEYA.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ARUSHA kituo cha THEMI Mkoa ARUSHA**
**Shauri la Ndoa Na 42 2024**
**Jina la madai TAMASHA YAHAYA MHAMALI**
**Jina la Mdaiwa NICODEMU FIKIRI**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa NICODEMU FIKIRI**
**NJIRO -0714 571448**

**Kwa kuwa Mdai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za Madai) UNATAKIWA KUFIKA MAHAKAMANI KUJIBU MADAI YA TALAKA NA MATUNZO YA WATOTO.**

Kwa hiyo wewe NICODEMU FIKIRI unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 10 Mwezi wa 10 Mwaka 2024 sas 3:00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea .

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini .Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 27 Mwezi 09 Mwaka 2024

**HAKIMU MKAZI.**

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA NZEGA**
**MAOMBI MADOGO NA. 16 NA 17 YA MWAKA 2024**

- **MASUNGA MOHAMED**
- **MALOMO MOHAMED**
- **AMOS MOHAMED**
- **KALIWA MOHAMED ............ WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

- **JUDITH HAULE**
- **SHIMBA MOHAMED............... WAJIBU MAOMBI**

**KUITWA SHAURINI**
Mjibu maombi SHIMBA MOHAMED popote ulipo unafahamishwa kwamba MASUNGA MOHAMED. NA WENZAKE 3 wamefungua maombi Madogo Na. 16 & 17 katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya lililopo Nzega. Shauri husika limepangwa kusikilizwa tarehe 15/10/2024 saa 2:30 asubuhi. Hivyo mnatakiwa kuleta utetezi wenu ndani ya siku 7 kuanzia tarehe ya kutolewa tangazo hili. Vielelezo vyote vya kesi vinapatikana katika Masjala ya wazi Baraza la Ardhi na Nyumba (W) – Nzega.

Ufahamu kwamba usipohudhuria maombi husika yatasikilizwa bila ya wewe kuwepo /kutoa utetezi wako na kutolewa hukumu.

IMETOLEWA na kutiwa saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 25/09/2024.

V. A.LING'WENTU
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
NZEGA

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LILIAN ALPHONCE MDUDA anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili T 726 EDL. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: PHQ/DAR/KIN/209053/2024.**

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**
**SHAURI LA MADAI NAMBARI 221 LA 2023**
**RONALD PHILIP FUNGAMTAMA...........MUOMBAJI/WAOMBAJI**
**DHIDI YA**

- **ELIJAH SAMSON MWAKILINDI**
- **MABUNDA AUCTIONEER MART CO. LTD...MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**

- **ELIJAH SAMSON MWAKILINDI (2) MABUNDA AUCTIONEER MART CO. LTD..............POPOTE ULIPO/MLIPO**

**RONALD PHILIP FUNGAMTAMA** amefungua/wamefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 07/10/2024 saa 3:00 asubuhi/mchana mbele ya J.W. SILLAS. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa Saini na Mhuri wa Baraza hii leo tarehe 25 Mwezi 09, 2024.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

---

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT, CAP 117 (R.E.20219)**
**DEED POLL ON CHANGE OF NAME**
**BY**
**LAIS LOMBAY KISSILA**

By this deed, I LAIS LOMBOY KISSILA,0766-773922- ARUSHA Do Hereby wholly and absolutely renounce, relinguish and abandon the use of my former name of LAIS KISSILA MOLLEL and in lieu thereof adopt as from the date of poll he name of LAIS LOMBOY KISSILA.

The reason for this change of name is I want to use the name that appears in the National identity card.

AND in pursuance of such change of name as aforesaid I hereby declare that I shall at all times hereafter in all records, deeds and instruments in writing and in all actions and proceedings and in all public and private dealings and upon all occasions whatsoever use and subscribe the name of LAIS LOMBOY KISSILA.

I hereby require and authorize all persons designate and describe me by the name of LAIS LOMBOY KISSILA In witness hereof I LAIS LOMBOY KISSILA have set my hand at ARUSHA this 5th day of February .2024.

Sworn and Delivered at Arusha by the said LAIS LOMBOY KISSILA who is known to me personally/identified to me by the later being known to me personally in my presence this 5th day of February, 2024.

Deponent



Name:
Signature:
Address:
qualification: Commissioner for Oaths

---

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

MOB: +255 - 0677020701

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,

WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Hezbollah yathibitisha kifo cha Nasrallah

**BEIRUT,** Lebanon

KUNDI la wanamgambo la Hezbollah la nchini Lebanon, limethibitisha kuwa kiongozi na mmoja wa waanzilishi wake, Hassan Nasrallah ameuawa katika shambulizi la anga la Israel siku ya Ijumaa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na kundi hilo linaloungwa mkono na Iran, Nasrallah na Katibu Mkuu wa Hezbollah, ameungana na mashahidi wenzake na wafiadini ambao aliwaongoza kwa takribani miaka 30.

Kupitia tarifa hiyo, Hezbollah iliapa kuendeleza vita vyake vitakatifu dhidi ya adui yake Israel na katika kuiunga mkono Palestina.

Jeshi la Israel lilisema Hassan Nasrallah aliuawa katika shambulizi sahihi la anga wakati wa mkutano wa viongozi wa kundi hilo kwenye makao yake makuu huko Dahiyeh, kusini mwa Beirut.

**Hezbollah bado wana roketi na makombora, na kundi hilo lina uwezo wa kuyarusha makombora mengi kwa wakati mmoja.**

"Hassan Nasrallah ameuawa," alitangaza msemaji wa jeshi la Israel, Luteni Kanali Nadav Shoshani, katika ukurasa wa mtandao wa X.

Duru karibu na kundi la Hezbollah limeliambia shirika la habari la Ufaransa, AFP kuwa mawasiliano na Nasrallah yalipotea tangu siku ya Ijumaa, wakati shambulizi lilipofanyika.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Ufaransa ilisema kulingana na taarifa walizo nazo ambazo zimethibitishwa, ni kweli Hassan Nasrallah ameuawa.

Aidha, Luteni Kanali Shoshani alisema bado wana kazi kubwa ya kufanya, na mapigano dhidi ya kundi la Hezbollah yanaendelea, hata baada ya kutangaza kumuuwa Nasrallah.

"Hezbollah bado wana roketi na makombora, na kundi hilo lina uwezo wa kuyarusha makombora mengi kwa wakati mmoja," alifafanua msemaji huyo wa jeshi la Israel.

Pia Luteni Kanali Shoshani alisema kundi hilo linaloungwa mkono na Iran, linaaminika kuwa na maelfu ya roketi, akieleza kuwa viongozi wengi wa ngazi ya juu wa Hezbollah pia wameuawa.

Jeshi la Israel IDF pia limesema limeyashambulia zaidi ya maeneo 140 ya Hezbollah tangu usiku wa Ijumaa.

"Tangu Ijumaa usiku, IDF ilishambulia ngome za kigaidi 140 za Hezbollah, ikiwemo mizinga inayotumika kuwalenga raia wa Israel, majengo ambayo silaha zinahifadhiwa, silaha za kimkakati, viwanda vya kutengeneza silaha, na maeneo ya ziada ya miundombinu ya kigaidi," taarifa ya jeshi ilieleza.

Naye mkuu wa majeshi ya Israel, Luteni Jenerali Herzi Halevi alisema Israel itaendeleza mashambulizi yake dhidi ya wanamgambo hao wa Hezbollah wanaoungwa mkono na Iran, hata baada ya mauaji ya Nasrallah.

"Kuuawa kwa Nasrallah sio mwisho wa mashambulizi yetu," alifafanua Luteni Jenerali Halevi.

Kundi la Hezbollah limesema linahusika na mashambulizi kadhaa ya makombora dhidi ya Israel. Huku ikielezwa kuwa Hezbollah, kundi la wanajeshi wa Israel walishambuliwa kwa mizinga kaskazini mwa Israel.

Hezbollah ilisema roketi lilirushwa kuelekea Kibbutz Sa'ar, na kwamba makombora zaidi yalirushwa katika kijiji cha Rosh Pina, ikiwa ni katika kulipiza kisasi dhidi ya mashambulizi ya kikatili ya Israel nchini Lebanon.

Kiongozi Mkuu wa kidini na mwenye mamlaka makubwa zaidi nchini Iran, Ayatollah Khamenei alilaani vikali kile alichokitaja kuwa sera ya 'kipumbavu na kijinga' ya utawala dhalimu wa Israel baada ya mashambulizi yake nchini Lebanon.

Khamenei amesema mauaji ya watu wasio na ulinzi nchini Lebanon kwa mara nyingine tena yanafichua ukatili wa Israel. **DW**

## Waliofariki kwa mafuriko Nepal wafikia 101

**KATHMANDU,** Nepal

TAKRIBAN watu 101 wamefariki na wengine 64 hawajulikani walipo nchini Nepal, kufuatia mafuriko na maporomoko ya ardhi yaliyosababishwa na mvua kubwa, hasa katika mji mkuu wa Kathmandu.

Kupitia taarifa ya Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini humo, Dan Bahadur Karki alisema jana kuwa hadi siku mbili zilizopita vifo vilikuwa ni 59, lakini hadi jana viliongezeka zaidi.

"Inawezekana kwamba idadi ya watu itaongezeka wakati kazi yetu ya utafutaji na uokoaji ikiendelea katika maeneo yaliyoathirika," alisema Karki. "Hii ndiyo mvua kubwa zaidi iliyorekodiwa katika mji mkuu tangu angalau miaka ya 1970," alisema Karki

Ilielezwa kuwa bonde la Kathmandu lilirekodi mvua ya milimita 240 kwa muda wa saa 24 kati ya Ijumaa na Jumamosi asubuhi.

Mamlaka ya hali ya hewa nchini Nepal imeliambia Gazeti la Kathmandu Post, kwamba hiyo ndiyo mvua kubwa zaidi iliyorekodiwa katika mji mkuu wa Nepal tangu angalau 1970, kulingana na shirika hili.

Aidha, ilielezwa kuwa mamlaka ilikuwa ikionya kuhusu mafuriko ya ghafla katika mito kadhaa wakati hali mbaya ya hewa ilipoanza. Na kwamba wakati huo mito ya Kathmandu ilifurika, ikasababisha mafuriko katika nyumba zilizo karibu na kingo.

Hata hivyo, baadhi ya walionusurika walikimbilia kwenye paa za majengo, wengine walikimbia kupitia maji ya matope. **RFI**




Waziri wa Afya wa Rwanda, Dk. Sabin Nsanzimana. **PICHA: MTANDAO**

# Sita wafariki kwa Marburg Rwanda

**KIGALI,** Rwanda

WAZIRI wa Afya wa nchini Rwanda, Dk. Sabin Nsanzimana amesema watu sita wamethibitishwa kufariki nchini humo kutokana na kuugua maradhi ya Marburg.

Taarifa hiyo inakuja baada ya Wizara ya Afya ya nchi hiyo kutangaza Septemba 27 mwaka huu kuwa ugonjwa huo umeripotiwa katika vituo mbalimbali vya afya nchini humo.

Kulingana na Nsanzimana, Jumla ya watu 20 wameugua na wengine sita wamepoteza maisha na kwamba wengi waliofariki na waliougua ni wafanyakazi wa vituo hivyo vya afya.

Dk. Nsanzimana alisema kuwa ugonjwa huo huambukizwa kwa njia ya damu na maji maji kutoka kwa watu wenye ugonjwa huo.

Pia ameongeza kuwa inaweza kuchukua hadi wiki tatu kwa aliyeambukizwa kutoonesha dalili zozote za ugonjwa huo.

"Ni ugonjwa hatari sana, kiasi kwamba yule aliyeambukizwa anaweza kupoteza uhai," alisema.

Virusi vya Marburg vinatajwa na wataalamu wa afya kuwa sawa na virusi hatari vya Ebola, vikiwa vimegunduliwa kwa mara ya kwanza mwaka 1967 nchini Ujerumani baada ya watu tisa kuambukizwa na saba kufariki dunia. **TRT**

HABARI MICHEZO

# WANAMAJI, BUBOMBI DIMBANI LEO NUSU FAINALI UMOJA CUP RORYA

**Na Mwandishi Wetu,**

RORYA

BAADA ya mtanange mkali wa nusu fainali ya kwanza ya michuano ya Umoja Cup Rorya 2024, kupigwa jana kati ya Kabwana FC na Gonga FC ya Busurwa, wapenzi wa soka wilayani hapa leo watashuhudia mechi kali ya nusu fainali ya pili wakati wenyeji na mabingwa watetezi, Wanamaji fc watakapowakaribisha Bubombi fc.

Mashindano hayo ya kila mwaka ya Umoja Cup Wilaya ya Rorya ambayo yanafanyika katika viwanja vya Maji Sota wilayani hapa, yalianza tangu Agosti mwaka huu yakishirikisha timu 18 kwa mfumo wa makundi manne kabla ya kufika hatua ya robo fainali na sasa nusu fainali.

Kabwana waliingia nusu fainali baada ya kuwafunga Masonga fc katika mchezo mkali wa robo fainali wakati Gonga fc wakiitoa Rifa huku Wanamaji fc wakiwafurumusha Shirati Mji na Bubombi fc wakiwatupa nje ya mashindano Mafundi fc kwa mikwaju ya penalti.

**Mwenyekiti wa mashindano hayo, Ochieng Meli, akizungumzia michuano hiyo juzi, alisema mdhamini wa ligi hiyo ya kila mwaka, Peter Owino, mwaka huu ameongeza zawadi kwa washindi.**

Meli alisema mshindi wa kwanza atapata seti moja ya jezi, kombe na pesa taslimu Sh. 500,000, wakati mshindi wa pili akiondoka na seti moja ya jezi na pesa taslimu Sh. 200,000

"Mshindi wa tatu yeye atazawadiwa seti moja na Sh.100,000, lakini pia mshindi wa nne hatatoka mikono mitupu kwani zawadi yake itakuwa jezi seti moja na Sh. 50,000," alisema.

Aidha, Melli alisema timu zote zilizocheza kuanzia hatua ya robo fainali zitazawadiwa mpira mmoja.

"Cha kutia moyo zaidi mwaka huu, kuna wadau wamejitokeza kumuunga mkono mdhamini wetu, Owino ambapo Joseph Ryangachi anayeishi Dar es Salaam, ameahidi kununua Kombe lenye thamani ya Sh. 300,000 kwa ajili ya mshindi wa kwanza huku Mwalimu Abele Kembo akitoa Sh.100,000 kwa timu itakayomaliza mashindano na mabao mengi pamoja na kocha bora wa mashindano.

"Pia Katibu wa Chama cha Mpira Miguu Wilayani Rorya, Charles Denis, ameahidi kutoa mpira kwa timu zitakazomaliza na mabao mengi," alisema.

Alisema timu yenye nidhamu itapata Sh. 30,000, mchezaji bora Sh. 40,000 na ngao, mfungaji bora Sh. 30,000 na ngao, kipa bora Sh. 30,000 na mchezaji chipukizi Sh. 20,000 huku pia ikitolewa tuzo kwa mtu mmoja kwa kutambua mchango wake kwa soka la Rorya.

Meneja wa Mashindano hayo, Daniel Maina, alisema mwaka huu walitegemea kujumuisha jumla ya timu 20, lakini mbili zilijitoa hivyo kubaki 18.

Kwa upande wa Katibu wa Umoja Cup, Teli Miki, amezikumbusha timu zote zinazoshiriki mashindano hayo ambayo ni maalum kwa ajili ya kuibua vipaji, kufahamu kuwa soka ni burudani na Umoja Cup mwaka huu inakwenda kwa kaulimbiu ya 'Umoja Wetu Ndio Nguzo Yetu'.



Kikosi cha Bubombi FC, kinachotarajiwa kushuka katika Uwanja wa Maji Sota, Rorya, kuwavaa wenyeji na mabingwa watetezi wa michuano ya Umoja Cup, Wanamaji fc, kwenye mechi ya nusu fainali ya mashindano hayo itakayopigwa uwanjani hapo leo. **MPIGAPICHA WETU**

## Namungo meno nje kuvunja mwiko Prisons

**Na Adam Fungamwango**

MCHEZAJI wa Namungo FC, Jacob Massawe, amesema yeye na wachezaji wenzake wamekuwa na furaha sana kuwa timu ya kwanza kuifunga bao Prisons msimu huu, lakini pia kupata ushindi baada ya misimu mitatu kupita dhidi yao.

Massawe ambaye ndiye mfungaji wa bao pekee la Namungo dhidi ya Prisons, katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliochezwa juzi, Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi, amesema haikuwa rahisi kuifunga timu ambayo kwa misimu mitatu wameshindwa kuchukua pointi tatu kutoka kwao, lakini pia kuvunja mwiko wa kutoruhusu bao kwenye ligi.

Ni msimu wangu wa tatu kuwapo Namungo na hatujawahi kupata ushindi wowote dhidi ya Prisons ni furaha sana kwa kweli, kumbuka walikuwa pia hawajaruhusu bao, leo tumevunja mwiko kwa kweli," alisema Massawe ambaye alipachika bao hilo dakika ya 71.

Prisons ilikuwa imecheza michezo minne bila kuruhusu bao na pia kufunga bao lolote, ikipoteza mechi hiyo kwa mara ya kwanza msimu huu.

"Niwashukuru wachezaji wenzangu, Prisons walianza kwa presha kubwa, lakini kila muda walikuwa wanashuka kutokana na jinsi tulivyokuwa tunawakabili.

"Kipindi cha pili tulibadilika na kwa sababu wao walichoka kwa nguvu walioitumia kipindi cha kwanza, basi tukaweza kushinda," alisema straika huyo ambaye pia alipata tuzo ya mchezaji bora wa mchezo.

Namungo imepata ushindi wake wa kwanza uwanja wake wa nyumbani baada ya michezo minne, ukiwa ni wa pili kwenye Ligi Kuu, ambapo wa kwanza iliifunga Coastal Union mabao 2-0, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

# Waendesha Baiskeli waanza safari Twende Butiama 2024

**Na Mwandishi Wetu**

WAENDESHA Baiskeli 113 wameanza safari ya kilomita 1,846 kutoka Dar es Salaam hadi Butiama kwa ajili ya Kampeni ya Twende Butiama 2024, wakiwamo washiriki wa kimataifa kutoka Kenya, Rwanda, Congo, Malawi, Zambia, na Burundi ambapo watapitia mikoa 12 kati ya Septemba 29 na Oktoba 13.

Msafara wa Twende Butiama , utaboresha maisha ya watu 100,000 watakaokutana nao njiani pamoja na kudumisha historia ya Tanzania huku lengo likiwa ni kumuenzi Hayati Mwalimu Julius Nyerere, Rais wa Kwanza wa Tanzania kwa vitendo kupitia kuendesha baiskeli mchezo ambao aliupenda.

"Twende Butiama inakusudia kupambana na maadui watatu wa maendeleo katika jamii: ujinga, umaskini, na maradhi. Huu ukiwa ni mwaka wake wa sita tangu kuanzishwa, msafara huu ambao unaakisi fahari ya kitaifa, ujasiri, na dhamira thabiti ya kuwahudumia wananchi, Kampuni ya Vodacom Tanzania imerejea kama mshirika mkuu kwa tukio la mwaka huu, ikipata msaada kutoka kwa wadau wengine kama Stanbic Bank Tanzania, YUNA, Kuunda, ABC Impact, na DarVelo Cycling"

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa msafara huo, Mkurugenzi wa Mahusiano na Vodacom Tanzania Foundation, Zuweina Farah, alisema; "Tunaamini katika kuleta maendeleo kupitia kuwawezesha watu na kutunza mazingira yetu.

"Mwaka jana, ushirikiano wetu na Twende Butiama ulifanikisha kupandwa miche ya miti 6,000, kuchangia madawati 610 kwa shule za msingi 13, na kutoa huduma za afya bure kwa zaidi ya watu 3,200 katika mikoa mitatu.

"Mwaka huu tumepata wadau wengine kuungana nasi kwa hivyo tuna imani tutafanya mengi zaidi kuboresha maisha ya Watanzania na kuenzi urithi wa Mwalimu."

Alisema msafara wa mwaka huo unatarajia kuchangia madawati 1,500 kwa shule zenye uhitaji, ikiwa ni pamoja na kutoa msaada wa vifaa saidizi kwa shule zenye wanafunzi wenye mahitaji maalum, pia utapanda miche 50,000 ya miti sambamba na kutoa elimu ya utunzaji wa mazingira.

"Mwaka huu msafara huu utawezesha kutolewa kwa kambi za matibabu katika mikoa yote 12 watakapokatiza ambapo watu watapata huduma za ushauri, uchunguzi, na matibabu bure. Msafara wa Twende Butiama, ulioanzishwa mwaka 2018 na wapenzi wa baiskeli wakiongozwa na Gabriel Landa, umekua kwa kasi, ukigusa maisha ya Watanzania wengi," alisema.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### DURAN AFUATILIWA

CHELSEA na West Ham ni miongoni mwa klabu zinazomfuatilia kwa karibu mshambuliaji wa Aston Villa na Colombia, Jhon Duran, 20. ***(Give Me Sport)***

### MURILLO SASA KUUZWA

KLABU ya Nottingham Forest itamuuza Murillo bila kutaka, ikiwa watapokea ada kubwa kwa beki huyo wa kati wa Brazil mwenye umri wa miaka 22, ambaye amekuwa akihusishwa na Barcelona na Real Madrid. ***(Football Insider)***

### BAENA AIVUTIA VILLA

WINGA wa Villarreal raia wa Hispania, Alex Baena mwenye umri wa miaka 23, amewavutia maskauti wa Aston Villa na Newcastle United msimu huu. ***(Caught Offside)***

### BAYERN WAITAMBIA UNITED

WAKUU wa Bayern Munich wanaamini kuwa walimsajili nyota wa pauni milioni 100 kwa nusu walipoishinda Manchester United kwenye usajili wa pauni milioni 50 wa winga wa Ufaransa, Michael Olise mwenye umri wa miaka 22 kutoka Crystal Palace. ***(Mirror)***

### POTTER NAYE ATAJWA

KLABU ya Southampton inaweza kumgeukia kocha wa zamani wa Chelsea na Brighton, Graham Potter iwapo wataamua kumfukuza, Russell Martin. ***(Football Insider)***

### EZE ARIDHIKA PALACE

WINGA wa England, Eberechi Eze, ameridhika na nafasi yake huko Crystal Palace, ambao walishangazwa kutopokea ofa kutoka kwa klabu za Ligi Kuu England wakati wa msimu wa majira ya joto. ***(Mirror)***

### WILSON KUONDOKA BURE

KLABU ya Newcastle United iko tayari kumruhusu mshambuliaji wa England, Callum Wilson, 32, kuondoka bila malipo msimu ujao iwapo hawatapata mbadala wake Januari. ***(Give me Sport)***

### YAZICI KUSAINI OLYMPIAKOS

MSHAMBULIAJI wa Uturuki, Yusuf Yazici, 27, anatazamiwa kusaini mkataba wa miaka mitatu na Klabu ya Ugiriki ya Olympiakos baada ya kuondoka katika Klabu ya Lille ya Ufaransa. ***(Fabrizio Romano)***

### PAZ AFUATILIWA MADRID

REAL Madrid inafuatilia hatua za Nico Paz, 20, huko Como na inaweza kukiamsha kipengele cha kumnunua mchezaji huyo wa Kimataifa wa Argentina ikiwa ataendelea kuonesha kiwango kizuri cha mchezo akiwa na timu hiyo ya Serie A. ***(AS)***

### DYCHE ATAKA KUBAKI

SEAN Dyche ameelezea wazi nia yake ya kutaka kubaki kama kocha wa Everton na kuwaongoza katika uwanja wao mpya, baada ya klabu hiyo kununuliwa. ***(Telegraph)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# GUARDIOLA: LAZIMA SASA NITAFUTE SULUHU YA RODRI

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amesema anahitaji "kutafuta suluhu" ya kukosekana kwa Rodri katika safu ya kiungo ya Manchester City baada ya mabingwa hao wa Ligi Kuu England kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Newcastle United Jumamosi.

**Rodri mwenye umri wa miaka 28, ameondolewa kwa muda wote uliosalia wa msimu huu baada ya kuumiza goti lake la kulia wakati wa sare ya mabao 2-2 dhidi ya Arsenal Jumapili iliyopita.**

Kabla ya safari ya Newcastle, City walikuwa wamepoteza mechi saba kati ya 21 za Ligi Kuu bila Rodri kucheza nafasi yake ya kawaida ya safu kiungo, wakati alisimamishwa msimu uliopita, kikosi cha Guardiola kilipoteza mechi mfululizo dhidi ya

> Ningependa awe hapa, lakini wakati mwingine hutokea na unapaswa kuzoea...

Newcastle na Wolves.

Lakini wakati City wakiepuka kichapo kwenye Uwanja wa St. James' Park, kiwango chao hakikuwa cha kuridhisha wakiwa na viungo Mateo Kovacic, Ilkay Gundogan na Rico Lewis.

"Jamani, najua mtaniuliza kila wakati, lakini yeye Rodri hayupo," alisema Guardiola. "Kova, Bernardo, Rico walifanya vema, lakini lazima nitafute suluhu. Ningependa Rodri awe hapa.

"Naiona timu yangu na kuitambua kikamilifu, tulikuwa na nafasi za kufunga na katika safu ya kiungo tulikuwa imara, suala lilikuwa mipira ya nyuma.

"Lakini wakati mwingine hutokea na unapaswa kuzoea. Tulipata nafasi za kufunga, lakini huu ni uwanja wao na walikuwa na nafasi za kufunga, kwa hiyo nina furaha."

Guardiola, wakati huo huo, alipunguza wasiwasi juu ya jeraha la mshambuliaji Erling Haaland wakati wa kipindi cha kwanza cha mchezo.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Norway alipata matibabu kwenye kifundo cha mguu wake wa kushoto, huku damu ikionekana kwenye soksi yake iliyochanika.

Lakini Haaland alimaliza mchezo na Guardiola alionekana kutokerwa na tatizo hilo alipoulizwa baada ya mchezo.

## HABARI MICHEZO

# PALMER AJISHANGAA KUTOFUNGA MATANO




**LONDON,** England

COLE Palmer alifunga mabao manne mbele ya Brighton & Hove Albion katika ushindi wa 4-2 wa Chelsea Jumamosi na mchezaji huyo wa Kimataifa wa England anaamini angeongeza zaidi kwenye mabao yake.

'The Blues' hao walipata ushindi mnono dhidi ya Brighton, huku mabao yote manne yakihusishwa na Palmer.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, aliendesha onesho kwenye pwani ya kusini, na kuwa mchezaji wa kwanza kufunga mabao manne katika kipindi cha kwanza katika historia ya Ligi Kuu England.

Hata hivyo, inaonekana manne hayo hayakumtosha Palmer, ambaye anaamini alipaswa kuifunga Brighton mabao matano au sita.

"Ningekuwa na tano au sita," alisema akiiambia BBC Match of the Day.


"Nilipokosa nafasi ya kwanza nilikasirika, lakini kwa jinsi walivyocheza na safu yao ya juu nilihisi tutapata nafasi nyingi zaidi.

"Kocha aliweka mpango mzuri wa mchezo, tulijua kuwashambulia kwa pasi za kwanza nyuma, Brighton ni timu nzuri, inapiga pasi vizuri, inacheza sawa na sisi, pointi tatu ndizo tulizozihitaji ndiyo maana tulichopata.

"Ninajaribu na kucheza kila mchezo kadri niwezavyo."

Pia alijibu maoni ya Theo Walcott kumfananisha na gwiji wa Arsenal, Dennis Bergkamp, ingawa alikiri kwamba alikuwa mdogo sana kuweza kumuona mchezaji huyo akicheza.

# Musiala aweka wazi msimamo wa kuhama



**MUNICH,** Ujerumani

KIUNGO wa Bayern Munich, Jamal Musiala, amekiri kuwa "niko wazi kwa kila kitu" huku tetesi za kuhamia Ligi Kuu England msimu ujao zikiendelea kuvuma.

Musiala ameingia katika miaka miwili ya mwisho ya mkataba wake na Bayern na amekuwa akihusishwa na kurejea England, ambapo Manchester City, Manchester United, Liverpool na waajiri wake wa zamani, Chelsea zote zikitajwa kumwania.

Hadharani, Musiala amekataa kukabidhi mustakabali wake kwa Bayern, licha ya maombi kadhaa ya wazi kutoka kwa wasimamizi wa Munich, na kwa mara nyingine tena amekiri kwamba uhamisho wake ujao haujaamuliwa licha ya maslahi makubwa ya Ligi Kuu.

"Hilo ni swali ambalo nimepata hapo awali," aliliambia The Times alipoulizwa kuhusu uwezekano wa kurudi England. "Kwangu mimi sina mpango wala nini, wewe chukua kinachokuja.

"Sijaribu kufikiria mbele sana juu ya mahali ninapotaka kuwa kwa sababu hali zinaweza kubadilika kila mwaka au kwa mwezi. Nikiwa na umri wa miaka sita, sikufikiria kuhusu England.

"Niko wazi kwa kila kitu, lakini nina furaha sana mahali nilipo sasa hivi."

Bayern hawajaficha nia yao ya kutaka kumsainisha Musiala mkataba mpya, huku rais wa klabu hiyo, Herbert Hainer, akizungumzia mapenzi yake kwa mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ujerumani.

"Lazima niseme kwamba tunampenda Jamal wetu kuliko kitu chochote," alisema Hainer akiiambia Abendzeitung.

"Yeye ni mwanasoka wa mara moja katika karne na lengo letu la kwanza bila shaka ni kumfunga FC Bayern kwa muda mrefu."

## Gordon apewa mkataba mpya Newcastle

**NEWCASTLE,** England

KLABU ya Newcastle United imeripotiwa kufikia makubaliano ya kuongeza mkataba na winga Anthony Gordon huku kukiwa na nia ya kutoka Arsenal na Chelsea.

Gordon alihusishwa kuondoka Newcastle wakati wa majira ya joto na ilidaiwa kuwa makubaliano yalifikiwa ya kumuuza mzaliwa huyo wa Merseyside kwenda Liverpool kwa pauni milioni 75 kabla ya 'Magpies' kufanikiwa kukusanya fedha kupitia kuondoka kwa Yankuba Minteh na Elliot Anderson.

Wakati dirisha la usajili lilipofungwa, Arsenal waliibuka kuwa wapenzi wa muda mrefu wa Gordon, lakini maofisa wa Newcastle waliweka wazi kuwa walikuwa na mipango ya kuongeza mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23.

Mazungumzo yalikumbwa na masuala machache, haswa kutokubaliana juu ya mshahara, lakini Daily Mail walikuwa wa kwanza kufichua mafanikio yalikuwa yamepatikana na na nyongeza sasa iko karibu.

Ripoti zinaeleza kwamba Gordon anatazamiwa kusaini mkataba mpya wa miaka sita ambao, muhimu zaidi hautajumuisha kifungu cha kutolewa.

Kocha Eddie Howe alikataa kuthibitisha habari za hivi punde kuhusu mustakabali wa Gordon, lakini hakuficha hamu ya klabu hiyo kutaka kumshikilia nyota huyo wa England.

"Tunampenda Anthony," alisema Howe. "Tungependa ajitolee maisha yake ya baadaye hapa. Tungependa abaki Newcastle kwa muda mrefu na kuendeleza mwanzo wake mzuri wa maisha yake hapa.



## Polisi Tanzania yalala tena nyumbani

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Polisi Tanzania imeendelea kupoteza mechi zake za Ligi ya Championship, ikicheza uwanja wake wa nyumbani wa Ushirika mjini Moshi, baada ya juzi kuchapwa bao 1-0 dhidi ya TMA.

Timu hiyo iliyoshuka daraja msimu wa 2022/23, ilipoteza mchezo wake wa kwanza wiki iliyopita kwenye uwanja huo huo ilipofungwa bao 1-0 dhidi ya Mbuni FC.

Matokeo hayo yanaifanya kuwa kwenye nafasi ya 15, ikiwa haina bao wala pointi.

Bao la wageni katika mchezo huo liliwekwa wavuni na Abdulaziz Shahame, dakika ya 52 na kuipeleka hadi nafasi ya tano ya msimamo.

Wakati maafande wa Polisi wakisuasua, Biashara United imepata ushindi wake wa pili ikicheza uwanja wake wa nyumbani, Karume, Musoma mkoani Mara.

Bao pekee lililofungwa na Januari Benson, limeifanya timu hiyo kujizolea pointi zote tatu na kufikisha jumla ya pointi sita, baada ya wiki iliyopita kupata ushindi kama huo dhidi ya Transit Camp.

Kwa ushindi huo, Biashara inashika nafasi ya tatu ya msimamo, ikiwa na pointi sita na mabao sita, katika ligi hiyo ambayo inaongozwa na Mtibwa Sugar ambayo Ijumaa ilipata ushindi wake wa pili kwa kuitwanga Cosmopolitan mabao 2-0.

Mechi nyingine ilichezwa Uwanja wa Higland, Morogoro, ambapo wenyeji, Green Warriors waliwakaribisha African Sports na kuwachapa bao 1-0.

Green Warriors ambao wiki iliyopita walipoteza kwa bao 2-0 dhidi ya Mtibwa Sugar, wanashika nafasi ya nane kwenye msimamo wa ligi hiyo.

# WADAU WA MICHEZO, WACHEZAJI WAKOSHWA TUZO ZA LIGI KUU NBC

**Na Mwandishi Wetu**

WADAU wa michezo wa mpira wa miguu nchini, wamesema utoaji wa tuzo mbalimbali zinazotolewa na Mdhamini Mkuu wa Ligi ya Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), umechochea kasi ya ushindani kwenye ligi hiyo huku Bodi ya Ligi nchini (TPLB), ikisisitiza uwapo wa ufanisi na umakini mkubwa katika upatikanaji wa washindi mbalimbali wa tuzo hizo.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti mwishoni mwa wiki wadau hao wakiwamo mashabiki, baadhi ya viongozi waandamizi wa mchezo huo nchini pamoja na baadhi ya wachezaji, wamesema pamoja na uwapo wa tuzo za mchezaji bora na kocha bora wa mwezi zilizokuwapo tangu msimu iliyopita ya ligi hiyo, ujio wa tuzo za mchezaji bora wa kila mechi za ligi hiyo umeongeza morali na ushindani kwa wachezaji.

Katika mahojiano yake na moja ya chombo cha habari hapa nchini mwishoni mwa wiki, Ofisa Mtendaji Mkuu wa TPLB, Almasi Kasongo, alisema washindi mbalimbali wa tuzo hizo wanapatikana kutokana na mchakato unaozingatia vigezo stahiki kupitia Kamati ya Tuzo ya Shirikisho la Soka nchini, TFF.

**“Nia hasa ni kuhakikisha tuzo hizi zinaleta tija iliyokusudiwa ambayo ni kuongeza morali kwa wachezaji na makocha wa klabu shiriki za ligi hii ili kuongeza ushindani. Hayo ndio malengo yetu na ndio ya mdhamini mkuu wa ligi hii Benki ya NBC kuwezesha wachezaji na makocha wahisi jitihada zao zinathaminiwa. Kwa kuzingatia hilo, kamati imekuwa makini sana kuhakikisha washindi wa tuzo hizi wanakuwa kweli wamestahili,” alibainisha,**

Kupitia maofisa wake mbalimbali ambao hukabidhi tuzo hizo kwenye michezo ya ligi hiyo inayochezwa kwenye viwanja mbalimbali hapa nchini, NBC imeonesha kuridhishwa kwa kiasi kikubwa na kasi ya ushindani inayoshuhudiwa kwenye ligi hiyo huku ikitaja uwapo wa tuzo hizo kama moja ya sababu za msingi katika kufanikisha ushindani huo.

Akizungumza wakati wa mechi kati ya Azam FC na Simba SC maarufu kama ‘Mzizima Derby’, iliyochezwa hivi karibuni kwenye Uwanja wa New Amaan Complex visiwani Zanzibar, Meneja wa Benki ya NBC Tawi la Zanzibar, Abdul Karim Mkila, alisema kutokana na muitikio chanya uliopatikana kupitia tuzo hizo, benki hiyo inajipanga zaidi ili kuendeleza ubunifu utakaoongeza mvuto zaidi wa ligi hiyo sambamba na kubuni huduma za kibenki mahususi zaidi kwa wadau wa michezo nchini.

”Ni faraja na heshima kwetu kuona kwamba wachezaji na makocha wanaopokea tuzo hizi wamekuwa wakifurahia na kujivunia. Furaha wanayoipata washindi hawa ni mrejesho kwetu kuwa wanaheshimu na kuthamini jitihada zetu katika maboresho tunayoendelea kuyafanya kwenye ligi zote tatu tunazozidhamini,” alisema Mkila, ambaye kwenye mchezo huo alikabidhi tuzo na fedha taslimu kiasi cha Sh. milioni moja kwa kwa kiungo wa Klabu ya Simba, Jean Charles Ahoua, aliyeibuka mchezaji bora wa Agosti.

Katika kuhakikisha kuwa zoezi la utoaji wa tuzo hizo linakuwa jumuishi zaidi, Mwenyekiti wa Chama Cha Soka Mkoa wa Dar es Salaam (DRFA), Lameck Nyambaya, pia alipata wasaa wa kukabidhi tuzo na fedha taslimu kiasi cha Sh. milioni moja kwa Kocha Mkuu wa Klabu ya Simba, Fadlu Davids, ambaye naye alitangzwa kuwa kocha bora wa ligi hiyo kwa Agosti.

Kama ilivyo kwa wachezaji wengine waliopata tuzo hizo, Kipa wa Simba, Moussa Camara, alieibuka mchezaji bora kwenye Derby hiyo ya Mzizima naye alikabidhiwa tuzo yake kutoka kwa NBC, na hakusita kuonesha furaha yake kupitia kurasa zake za mitandao ya kijamii ambapo alionekana katika picha akiwa kwenye ‘mapozi’ tofauti ikiwamo kulala kitandani akiwa ameshikilia tuzo hiyo.




Meneja wa Benki ya NBC Tawi la Zanzibar, Abdul Karim Mkila (Kushoto), akikabidhi tuzo kwa Kiungo wa Klabu ya Simba, Jean Charles Ahoua, aliyetangazwa mchezaji bora wa Ligi Kuu ya NBC kwa Agosti, wakati wa mechi kati ya Azam FC na Simba iliyopigwa kwenye Uwanja wa New Amaan Complex, Zanzibar wiki iliyopita. Simba iliibuka na ushindi wa mabao 2-0. **MPIGAPICHA WETU**

## *Daktari afichua sababu majeruhi*

INATOKA UK. 24

saidia kucheza michezo mingine kama kuogelea, tenisi na mingine kupunguza fatiki, pia kuwapunguzia dakika za kucheza, ndiyo maana unaona kuna wakati kocha anabadilisha kikosi, au anapanga fulani acheze halafu atoke, baadaye aingie mwingine,” alisema.

Timu za Simba na Yanga zimeonekana kuathirika zaidi kwa hili, kwani zimetoka kucheza michezo ya kimataifa hivi karibuni na moja kwa moja zimeanza kucheza michezo mfululizo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Wakati huo huo, daktari huyo amesema mchezaji Farid Mussa anaendelea vizuri na huenda wiki ijayo kaanza mazoezi mepesi.

Hata hivyo, amebainisha itachukua kiasi cha miezi miwili au mitatu kuwa fiti kabisa na kurejea uwanjani.

“Kama tulisema alifanyiwa upasuaji mkubwa wa nyama za nyuma ya goti, kuna msuli ulikuwa umekatika kwa hiyo tulifanya hivyo ili kuurudishia sehemu yake, wiki inayokuja ataanza mazoezi mepesi ya gym, na baada ya miezi miwili atakuwa tayari ameshapona na mwezi mmoja ataanza mazoezi ya kuweka mwili wake kwenye hali ya utimamu ili kuweza kurejea uwanjani, kwa maana hiyo itachukua miezi miwili au mitatu,” alisema Etutu.

## Kibu aitamani Yanga mapema

INATOKA UK. 24

Mechi zote hizo, Kibu alifunga mabao, akipachika bao la pili katika mechi ambayo Simba ilishinda 2-0 na bao la kufutia machozi ilipofunga 5-1, lakini hakuweza kumaliza baada ya kufanyiwa madhambi.

“Kwa hiyo naisubiri kwa hamu ili niwathibitishie mashabiki wa Simba kuwa mimi niko na wao,” alisema.

Kibu pia aliuzungumzia mchezo wao dhidi ya Al Ahli Tripoli uliochezwa hivi karibuni kuwa ulikuwa mgumu mno tofauti na wengi walivyofikiria.

“Hata lile bao ukiangalia lililifunga kwenye mazingira magumu, lilikuwa gumu, halikuwa rahisi kufunga, lakini haikuwa rahisi kuuzuia ule mpira, nilishukuru sana kufunga lile bao, ila niseme hakukuwa na muda wa kushangilia,” alisema.

# Michezo

Jumatatu Septemba 30, 2024

Nipashe





Palmer ajishangaa kutofunga ma5

UKURASA 22

# DAKTARI AFICHUA SABABU WACHEZAJI MAJERUHI LIGI KUU

●●● Atoa tahadhari akitaka ratiba ya Ligi Kuu imulikwe kupunguza kucheza karibu karibu, huku...

**Na Adam Fungamwango**

DAKTARI wa Yanga, Moses Etutu, amesema mechi mfululizo zinawafanya wachezaji wengi kuwa majeruhi bila kuumizwa, hivyo kushauri wawe wanacheza mechi moja kwa wiki.

**Akizungumza jijini Dar es Salaam, Etutu, amesema mechi ambazo wachezaji wanacheza mara mbili kwa wiki na kufululiza wiki hadi wiki, zinasababisha uwezekano wa kuchanika kwa nyama za misuli.**

Alisema mchezaji wa mpira wa miguu ili kuepuka majeraha ambayo si ya kuumizwa na wenzake, anapaswa kucheza mechi moja kwa wiki moja.

"Sisi kama madaktari tunashauri angalau mechi moja kwa wiki, lakini baada ya saa 72 muda unakuwa mchache wachezaji wanakuwa na 'fatiki' ambazo zinawasababishia kupata majeraha mengine kama kuchanika kwa nyama za misuli, ila kuna zingine haziepukiki.

"Mfano mtu amekuchezea rafu au amekukanyaga, hizi mchezaji anaweza kuzipata hata akikaa mwezi mzima bila kucheza, lakini hizi za kucheza mfululizo ni hatari, wachezaji wanatumia misuli, wanatumia nguvu, kwa hiyo nyama zinachanika," alisema daktari huyo.

Aliongeza kuwa hata uchovu wa kucheza michezo mingi pia inasababisha wachezaji kupata majeraha.

"Mtu anaweza kukuchezea vibaya na kama ukiwa fiti ungeweza kuepuka kwa kuruka, lakini unakuta misuli imechoka kutokana na uchovu wa kucheza mechi nyingi, unashindwa kufanya hivyo, unaumia, hivyo kila mechi zinazokuwa zimekaribiana na kuwa nyingi, uwezakano wa kupata majeraha unakuwa mkubwa sana," alisema.

Alisema wao kama Yanga wanajaribu kupunguza kwa kushirikiana na benchi la ufundi.

"Tunafanya ili kusaidia kuepuka majeraha kwa hiyo hapa inatakiwa ushirikiano wetu madaktari, kocha mkuu na kocha wa viungo, tunafanya kazi pamoja ili kuweza kusaidia kupunguza hili kwa kuwapa matibabu, pamoja na kuwa-

INAENDELEA UKURASA 23




Kibu Denis

# Kibu aitamani mechi Yanga mapema

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI mechi ya watani wa jadi ikitarajia kuchezwa Oktoba 19, mwaka huu, winga wa Simba, Kibu Denis, amesema anatamani siku ifike upesi kwani anapenda sana kucheza mechi za dabi.

Kibu, ambaye hivi karibuni aliingia kwenye mzozo na klabu yake kwa kutoroka kwenda nje ya nchi kwa ajili ya kujaribu kucheza soka la kulipwa kabla ya kurejea, alisema moja ya mechi ambazo anapenda sana kucheza ni dhidi ya Yanga.

Amebainisha kuwa mara nyingi 'dabi' ikifika yeye anakuwa kwenye wakati mzuri sana, na anakuwa na hamu ya kutaka kuwaonesha mashabiki nini anakitoa kwa timu yake.

"Mimi katika mechi ambayo huwa napenda zaidi kucheza ni dhidi ya Yanga, yaani mchezo wa 'dabi' wa timu hizi mimi ndiyo nazipenda sana kuliko zingine, kwa hiyo naisubiri kwa hamu," alisema mchezaji huyo ambaye alisajiliwa akitokea Mbeya City mwaka 2021.

Alibainisha hata kuumia mara kwa mara katika michezo baina ya timu hizo, inatokana na jinsi anavyojitolea, lakini hana ugomvi na mtu kwani yanayotokea yote ni mambo ya soka.

"Ni mechi ambazo huwa zikifika na mimi natakiwa kucheza huwa niko kwenye 'mudi' sana, nakuwa nimejiandaa vizuri nataka niwaoneshe mashabiki uwezo wangu na huwa najitoa, napambana hadi tone la mwisho la damu.

"Nafikiri hata ninavyoumia ni kwa sababu hiyo, nakumbuka nilivyogongana na Kibwana Shomari mechi moja, na ile ambayo niliumizwa na kipa wa Yanga, Djigui Diarra.

Kibu aligongana na Kibwana katika mchezo wa raundi ya pili ya Ligi Kuu Tanzania Bara uliochezwa Aprili 16, 2023, msimu wa 2022/23, Simba ikishinda mabao 2-0 na wote wawili walipata majeraha.

Mchezaji huyo pia aliumizwa na kipa Diara katika mechi ya raundi ya kwanza msimu uliopita uliochezwa, Novemba 6, mwaka jana, Yanga ikishinda mabao 5-1.

INAENDELEA UKURASA 23


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042